3000/-

# UWEZO WA LUGHA KATIKA MATINI YA SIASA NCHINI KENYA KUANZIA MWAKA 2002 HADI 2005.

MARGAN CARLPETERS ADERO

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu cha Kenyatta.

2005

Adero, Margan
*Uwezo wa lugha katika matini ya*
2006/279844

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.

**MARGAN CARLPETERS ADERO**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa chuo kikuu cha Kenyatta

**DKT. SHEILA RYANGA**

**Na**

July 13, 2005

**PROF. IRERI MBAABU**

## YALIYOMO

Yaliyomo ........................................................................................ i

Tabaruku ........................................................................................ v

Vifupisho ........................................................................................ vi

Shukrani ........................................................................................ vii

Ikisiri ........................................................................................ viii

Maelezo ya dhana muhimu ........................................................ ix

## SURA YA KWANZA

1.0 **Utangulizi** ........................................................ 1

1.1 Swala la utafiti ........................................................ 4

1.2 Malengo ya utafiti ........................................................ 5

1.3 Sababu za kuchagua mada ........................................ 5

1.4 Misingi ya nadharia na mihimili yake ........................ 6

1.5 Yaliyoandikwa kuhusu mada ...................................... 7

1.6 Mbinu za utafiti ........................................................ 10

1.7 Upeo wa utafiti ........................................................ 11

1.8 Uchanganuzi wa data ................................................ 12

## SURA YA PILI


**2.0 Lugha, Siasa, Mamlaka na Itikadi** .......................... 13

2.1 Utangulizi .......................... 13

2.2 Lugha .......................... 13

2.3 Uhusiano wa mamlaka na lugha .......................... 19

2.4 Lugha ya siasa .......................... 20

2.5 Siasa .......................... 21

2.6 Itikadi .......................... 22

2.7 Lugha na Itikadi .......................... 25

2.8 Mamlaka .......................... 25

2.9 Hitimisho .......................... 30


## SURA YA TATU


**3.0 Uchanganuzi wa Data ya Hotuba ya Siasa** .......................... 31

3.1 Utangulizi .......................... 31

3.2 Tamathali za ufananisho .......................... 35

3.3 "Mbwa Wa Kisiasa" .......................... 38

3.4 Kejeli .......................... 38

3.5 Sitiari .......................... 39

3.6 Vijembe .......................... 41

3.7 Mwingiliano wa matini katika siasa .......................... 41

3.7.1 Urejeshaji .......................... 42

| | | |
|---|---|---|
| 3.7.2 | Ubadilishaji | 43 |
| 3.7.3 | Udondoshaji | 43 |
| 3.7.4 | Mshikamano wa kileksia | 43 |
| 3.7.5 | Uunganishaji | 44 |
| 3.8 | Maelezo | 47 |
| 3.8.1 | Eksofora | 47 |
| 3.8.2 | Visawe | 47 |
| 3.8.3 | Maudhui | 48 |
| 3.8.4 | Ufafanuzi | 48 |
| 3.8.5 | Ufafanuzi Elezi | 49 |
| 3.8.6 | Hitimisho | 49 |

**SURA YA NNE**

| | | |
|---|---|---|
| **4.0** | **Dhima ya Lugha Katika Matini ya Siasa Nchini Kenya** | **50** |
| 4.1 | Utangulizi | 50 |
| 4.2 | Ahadi | 51 |
| 4.3 | Matumaini | 53 |
| 4.4 | Uchochezi | 54 |
| 4.5 | Kutahadharisha | 55 |
| 4.6 | Kuzindua | 56 |
| 4.7 | Changamoto | 58 |
| 4.8 | Katiba | 61 |

4.9 Utata wa Lugha Fiche .......... 66

4.10 Nyimbo na miito ya siasa .......... 67

4.11 Hitimisho .......... 70

## SURA YA TANO

**5.0 Hitimisho** .......... 71

5.1 Utangulizi .......... 71

5.2 Matokeo ya Utafiti .......... 71

5.3 Mapendekezo ya Utafiti zaidi .......... 77

5.4 Matatizo .......... 77

Ratiba .......... 78

Marejeleo .......... 80



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa Cecilia Atieno na kwa watoto wangu Jane, Chris, Nicholas na Levina.

Naitabarukia kazi hii pia kwa marehemu babangu Alex Adero Sumba, ndugu yangu Nicholas Peter Adero, mamangu Hendrica Magani na dada zangu Mathilda Lobo na Consolata Namanjaba. Maulana aweke roho zao mahali pema peponi.

Mwisho ni kwa Lucas Mandu Hainja kwa kunipa shinikizo ili niendeleze kisomo changu.

**VIFUPISHO**

| | | |
|---|---|---|
| NAK | - | National Alliance of Kenya |
| NARC | - | National Alliance Rainbow Coalition |
| KANU | - | Kenya African National Union |
| LDP | - | Liberal Democratic Party |
| KTN | - | Kenya Television Network |
| DP | - | Democratic party |
| NPK | - | National Party of Kenya |
| MOU | - | Memorandum of understanding |
| KBC | - | Kenya Broadcasting Corporation |

## SHUKRANI

Ningependa kumshukuru Maulana kwa kunipa siha njema kuendeleza masomo yangu.

Ninatoa pongezi zangu kwa Prof. Ireri Mbaabu na Dkt. Sheila Ryanga kwa ushauri wao na pia kwa kunisimamia katika utafiti huu.

Nawashukuru wahadhiri wangu Mwenyekiti Bwana Mugambi, Dkt. Mathooko, Dkt. Momanyi, Mwalimu Gathenji, Prof. King'ei na Dkt. Wafula wote wa idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa kunifunza na kunielekeza katika usomi.

Ninatoa shukrani zingine kwa Bwana Benard Mwiso na Hamisi Babusa kwa mijadala tuliyofanya pamoja ili kuandika tasnifu hii.

Shukrani kwa Ali Mtenzi wa K.T.N, Zachary Githathi wa Nation, kwa kunipa kanda za video nilizotumia katika utafiti huu. Bwana Peter Were mkutubi wa gazeti la Standard kwa kunipa magazeti niliyoyasoma ili kufanya utafiti huu. Ninawashukuru pia wanafunzi wote wa idara ya Kiswahili kwa mijadala tuliyofanya darasani na mawaidha yao kuhusu kozi nzima ya uzamili.

Shukrani zangu, pia, ziwaendee Bw. Obure Phillippé, Okeloh Wa Namadoa na Muswali Gabriel kwa kunisadia katika uchapishaji wa kazi hii.

## IKISIRI

Utafiti huu unaangazia uwezo wa lugha katika matini ya siasa nchini Kenya. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kudhihirisha vile lugha hutumiwa na wanasiasa ili waweze kuonyesha itikadi zao na pia kupata mamlaka. Ili kuonyesha uwezo wa lugha katika matini za siasa nadharia ya uchanganuzi usemi hakiki ndio imetumiwa.

Katika utafiti huu sura ya kwanza ambayo ni utangulizi wa tasnifu inashughulikia swala la utafiti, sababu za kuchagua mada, nadharia, madhumuni, upeo wa utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti. Sura ya pili inaangazia na kueleza dhana muhimu zilizotumiwa katika utafiti. Pia inaelezea mwingiliano uliopo kati ya lugha, siasa, mamlaka na itikadi.

Sura ya tatu inahusu uchanganuzi wa data ya hotuba za kisiasa na kuzichanganua kimuktadha na kimaana. Inatoa maelezo ya hotuba zilizotolewa katika kipindi cha siasa kinachozungumziwa. Sura ya nne ni uchanganuzi wa data na kueleza uwezo huo wa lugha katika hotuba za kisiasa nchini Kenya. Sura ya tano ni matokeo ya utafiti, mapendekezo ya utafiti mwingine na matatizo yaliyoukumba utafiti.

# MAELEZO YA DHANA MUHIMU

## LUGHA

Ni mfumo wa ishara ambazo zinatumiwa na watu kuwasiliana. Ishara zinazotumiwa na lugha ni zile ambazo zinaweza kuitwa taashira. Taashira ni ishara ambazo watumizi hukubaliana na kuzipa maana katika muktadha fulani.

## SIASA

Dhana inayotumiwa kuelezea mfumo wa uendeshaji wa masuala ya kijamii katika taifa au taifa dola. Huweza kuhusisha mkabala mfumo wa vipengele vya kijamii, kiutamaduni, kiuchumi. Siasa hujihusisha na maswala ya mitafaruku na mbinu ya utatuzi wa mitafaruku hiyo. Migongano hiyo inaweza kuhusu mitazamo mbalimbali, thamani, dini, makabila au utamaduni ambayo yote hii inaweza kusababisha migogoro katika jamii.

## MATINI

Matini ni taarifa yoyote ya maandishi au mazungumzo inayoweza kujisimamia katika kuelezea wazo na kujibainisha. Ni aina yoyote ya mazungumzo na yanaweza kuwa na urefu wowote mradi tu yaunde usemi ulio kamili. Matini inaweza kuandikwa kwa lugha ya nadhari au ya kishairi, inaweza kuhusisha mazungumzo ya mtu mmoja (monolojia) au ihusishe mazungumzo ya watu wawili au zaidi (dayolojia).

**MAMLAKA**

Mamlaka ni uwezo wa kufanya mambo kutendeka iwapo watu watakubali au la. Kwa hivyo walioamriwa watafanya majukumu waliopewa hata ikiwa hawataki kufanya.

**ITIKADI**

Ni mawazo makuu yanayotawala mtazamo wa mtu kuhusiana na maisha kwa ujumla na jinsi mawazo hayo yanavyotusaidia au kutukwamisha katika juhudi zetu za kutatua matatizo ya ulimwengu wetu tulionao.

Itikadi hutofautisha watu mbalimbali kwa mfano mmoja anaweza kuona kwamba matatizo mbalimbali yanayotokea katika ulimwengu wetu yana vyanzo vinavyoeleweka na kuweza kuelezwa ilhali mwingine akaona kuwa matatizo ya ulimwengu huu hayawezi kuelezeka kwa sababu yanathibitiwa na nguvu tusizoziona.

**MAZINGIRA**

Katika utafiti huu neno mazingira limetumiwa kumaanisha jumla ya vitu vinavyozunguka mwanasiasa na kumwathiri.

# *SURA YA KWANZA*

## 1.0 Utangulizi

Madhumuni ya utafiti huu ni kuchunguza uwezo na matumizi ya lugha kama vile inavyotumiwa na wanasiasa kwa manufaa yao. Lugha ya kisiasa ina mvuto na huwasilishwa kwa njia tofauti tofauti na wanasiasa. Lugha ni muhimu katika kuwawezesha wanasiasa kuimarisha mawasiliano yao. Ingawa maneno wanayoyatumia huwa ya kawaida lakini huonekana ya ughaibuni. Mtindo wa maongezi wanaotumia wanasiasa huwajenga wahudumu na kuwabomoa wapinzani wao.

Lugha ya siasa kwa jumla imewavutia wasomi mbalimbali na ni swala linaloibua hisia mbalimbali wakati linapozungumziwa. Swala hili limezingatiwa na wanaisimu na wanahistoria miongoni mwa wengine. Ingawaje ni vigumu kuzungumzia maswala ya siasa bila ya kuingilia siasa zenyewe, tumezingatia desturi za matini za kisiasa katika muktadha wa kiusomi. Van Djik (2000) alisema kuwa matini za kisiasa huathiriwa na miktadha mbalimbali ikiweko hali ya kisiasa, miundo na matukio.

Kabla ya mwaka wa 2002, chama kilichotawala nchini Kenya ni cha KANU. Chama hiki kiliundwa mwaka wa 1960 na ndicho kilichotawala nchi ya Kenya baada ya uhuru mwaka wa 1963 ambapo Rais wa kwanza alikuwa Hayati Mzee Jomo Kenyatta. Baada ya kifo chake, aliyechukua hatamu za uongozi alikuwa Rais Daniel

arap Moi, aliyeongoza chama cha KANU na nchi ya Kenya kuanzia mwaka wa 1978 hadi 2002. Rais Moi alimteua Uhuru Kenyatta ili awanie uongozi wa nchi kwa tikiti ya chama cha KANU dhidi ya kiongozi wa upinzani, Mwai Kibaki.

Kulikuwepo na misamiati iliyotumiwa na wanasiasa wakati huo huo ili kusuta wapinzani, kuwakejeli, kuwalaani na kuwasisimua wafuasi. Vyama vya upinzani pamoja na wakereketwa wengine wa mageuzi wa wakati huo pia walikuwa na lugha yao iliyokithiri lugha ya aina yake, iliyonuiwa kuwaelimisha, kuzindua na kuwapa changamoto wananchi. Wananchi walilalamika ili kuonyesha maovu yaliyofanywa na chama tawala cha wakati huo cha KANU. Huu ndio muktadha uliozalisha utafiti huu. Tulinuia kuchanganua jinsi lugha inavyoweza kunyumbishwa na watumiaji wake, na mambo tofauti tofauti yanavyoathiri unyumbuaji wa lugha. Vyama vya upinzani vilikuwa na miito yao ilhali kile cha KANU kikawa na mwito wa Harambee:

| | |
|---|---|
| Mwito: | *Harambee-eee-eee-ee* |
| Kiitikio: | *Nyayo-ooo-ooo-oo* |
| Mwito: | *Moi wapiiii-iii-iii?* |
| Kiitikio: | *Juuu-juuu-juuu, Juu zaidi!* |

Muungano wa vyama vya upinzani nao ukaja na mwito wake (*NARC! Mwenge*)

| | |
|---|---|
| Mwito: | *NAAA-AARC* |
| Kiitikio: | *Mwenge-eee-eee-ee* |



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Aidha mwito wa 'yote yawezekana' bila watu fulani katika utawala uliokuwepo kwa mfano; Yote yawezekana bila Moi.

Kando na vyama, wanasiasa pia walikuwa na lugha zao binafsi katika kampeni, msamiati mpya ukaibuka wakati huo, huku wanasiassa wakijizatiti kutafuta mamlaka; kwa mfano Reuben Ndolo aliposema "ukiwaona wao"; Raila alipotangaza "mpira" na Dkt. Mukhisa Kituyi alipoimba "wimbo wa mungiki".

Baada ya kura za mwaka wa 2002, matumizi ya lugha kwa kiwango kikubwa yalibadilika. Mabadiliko hayo yalikuwa kwa minajili kubwa ikiwa ni kukimu mahitaji ya vyama na wanasiasa kwa wakati huu. Upande wa serikali ya NARC nayo ikabadilisha usemi. Iliyojumuisha maswala ya ufufuzi wa uchumi, uwekezaji, maadili, ufisadi, usalama, haki za kibinadamu, ugonjwa wa ukimwi na umaskini. Kwa kiwango kikubwa matumizi ya lugha iliyonata kuhusu maswala hayo ilinuiwa kuwashawishi wananchi wawapigie kura ili kupata mamlaka. Hivyo basi, ilibainika wazi kuwa lugha katika matini ya kisiasa kuanzia mwaka wa 2002 (kabla na baaada ya uchaguzi mkuu) ilizaliwa, ikakua na ikafa kulingana na matakwa na mahitaji tofauti. Hivyo usemi wa kisasa, ilipitia metamofosisi fulani. Mabadiliko hayo yalikuwa na mafunzo kuhusu lugha ya siasa kuanzia mwaka wa 2002.

Kwa hivyo, kwa kutumia lugha, wanasiasa walinyang'anyana uwezo na mamlaka baina yao na vile vile walinyakua mamlaka hayo kutoka kwa watu na huiweka

katika kilinge cha uongozi pale watu wachache walithubutu kufikia. Wanasiasa walikuwa na njia tofauti za kutumia lugha bila wao kutaja wazi na hivyo huweza kuhimili maongezi ya kisiasa. Wanasiasa waliofaulu walikuwa na uwezo wa kutambua udhaifu wa maongezi hayo. Wao walitumia mbinu hizi ili kuwasilisha ujumbe wao na kupata wafuasi wengi, hata ikiwa wakati mwingine walisema uongo bora lugha waliyoitumia iliwapendeza na kuwavutia watu wengi.

## 1.1 Swala La Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kuonyesha uwezo wa lugha katika kuendeleza matamanio ya wanasiasa ili wapate mamlaka. Kuna aina mbalimbali ya mamlaka; ya kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Ingawaje utafiti mwingi ulifanywa kuonyesha vile muktadha huathiri matumizi ya lugha, utafiti huu utapiga hatua ili uweze kudhihirisha kuwa mtazamo wa kiitikadi wa wanasiasa ni kigezo muhimu ambacho wanasiasa hutumia na hivyo kuchagua lugha maalum ili kuwasilisha ujumbe walio nao. Kwa hivyo wanasiasa hutumia lugha kiitikadi ili kupata mamlaka kwa watu au jamii kwa ujumla.

Utafiti huu ulijaribu kujibu maswali yafuatayo:

1. Itikadi huchangia vipi malengo ya wanasiasa?
2. Kuna uhusiano gani kati ya matumizi ya lugha na udhibiti wa mamlaka ya wanasiasa?
3. Wanasiasa huathiriwa vipi na matarajio ya umma?

## 1.2 Malengo Ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo yafuatayo:-

1. Kuonyesha jinsi wanasiasa wanavyobainisha mtazamo wao kwa kujitetea na kupinga kwa kutumia maneno au lugha.
2. Kuthibitisha kuwa lugha husaidia kuweka na kujenga misingi ya itikadi na mielekeo ili kuwadumisha wanasiasa na jamii kwa jumla.
3. Kubainisha kuwa umilisi wa wazungumzaji au wanasiasa unategemea ujuzi wao na uhusiano uliopo kati ya lugha na mamlaka.

## 1.3 Sababu Za Kuchagua Mada

Utafiti huu ulitokana na mshawasha wa mtafiti ambaye alivutiwa kwa miaka kadha na umilisi wa lugha ya wanasiasa. Wanasiasa huelezea dhana za kawaida kwa njia tofauti sana na hivyo kutumia lugha mahsusi ili kueleza ujumbe wao. Itikadi za wanasiasa zina umuhimu gani kwao ili kuwawezesha kuwa na mamlaka? Kuchochea na maongezi ya wanasiasa ambapo wana kipawa cha kuweza kutumia lugha kwa umahiri. Pia kuchunguza kwa nini hadhira huvutiwa na aina ya uneni wa wanasiasa na hivyo hadhira humiminika kwa wingi ili kuwasikiliza, na athari za hotuba na matini hizi kwa jamii. Kwa hivyo, uwezo wa wanasiasa kuweza kuteua lugha maalum ili kuwasilisha ujumbe wao, ndilo jambo lililozaa utafiti huu.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## 1.4 Misingi Ya Nadharia Na Mihimili Yake.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uchanganuzi usemi hakiki. Fairclough (1994) ndiye mwasisi wa nadharia hii na anaeleza kwamba inaitwa uchanganuzi usemi hakiki kwa sababu lengo lake ni kuonyesha mwingiliano na mahusiano ambayo yanaweza kuwa yamefichwa yasionekane na watu, kwa mfano mwingiliano baina ya lugha, mamlaka na itikadi. Nadharia hii inajihusisha na mahusiano kati ya matumizi ya lugha na uwezo.

Kwa mujibu wa Crystal (1997), uchanganuzi usemi hakiki ni dhana ya kuonyesha uhusiano kati ya matukio ya kiusemi, siasa jamii na utamaduni; hasa kuambatana na vile usemi unavyoathiriwa na itikadi na vile usemi wenyewe unaweza kuathiri matukio katika jamii. Dijk (1998) naye, ameeleza kwamba nadharia hii inahusiana na kusaili mielekeo ya usemi inayohusu matumizi ya nguvu, udhalimu na utabaka unaotokana na matumizi mabaya ya mamlaka yaani ile mielekeo ya usemi ambayo huunda, hudumisha au kurudufisha hali ya watu katika jamii.

Bright (1920) anafafanua uchanganuzi usemi hakiki kama uchanganuzi wa matini kuhusiana na muktadha wake wa kijamii kuhusu uzalishaji wa matini na ufafanuzi. Mesthrie (2000) anasema kwamba lengo kuu la uchanganuzi usemi hakiki ni uchanganuzi wa sampuli za lugha ili kuweka wazi namna ambavyo lugha, hudumisha au kurudufisha hali ya watu katika jamii. Hii ni kwa sababu lugha hazitoshani na kuna haja ya kutetea lugha za wachache.

Scotton (1993) ameeleza jinsi lugha inavyoweza kutumiwa kuonyesha hadhi ya mtu na kwamba wazungumzaji wakiwa katika mazingira tofauti wanaweza kubadili msimbo ili kukidhi mahitaji yao, na kwamba lugha inaweza kutumiwa kama kigezo cha kupimia mamlaka waliyo nayo watu.

Ifuatayo ni mihimili yake:

1. Kusaidia kukosoa upuuzaji na umuhimu wa lugha katika kuzalisha mahusiano ya kijamii kuhusiana na mamlaka.
2. Kusaidia watu kuelewa jinsi lugha inavyochangia kutawaliwa kwa baadhi ya watu na wengine kwa vile utambuzi huu huwa ni hatua ya kwanza ya kujikomboa na hivyo kuangazia uwezo wa lugha.

## 1.5 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Lwaitama (1988) alifanya utafiti kuhusu hotuba za kisiasa katika Kiswahili. Aliandika kuhusu mtindo wa maongezi ya wanasiasa nchini Tanzania ambao ni Marais wa hapo zamani, Mwalimu Julius Nyerere na Ali Hassan Mwinyi. Aligundua kuwa utumiaji wa njia mbalimbali za viwakilishi nomino sio tu wa mtu binafsi, bali pia hutegemea muktadha. Mwinyi na Nyerere walitumia viwakilishi nomino katika nafsi ya kwanza kwenye miswada ya maongezi (kunena) kuliko miswada iliyoandikwa. Nafsi ya pili ilitumiwa na wahusika wote (Nyerere na Mwinyi) wakati walipoangazia kuhusu uraimishaji wa mamlaka. Utafiti huu ulishughulikia

muktadha na leksikografia tofauti na utafiti wetu ambao ulizingatia itikadi na jinsi wanasiasa wanavyotumia lugha kuelezea dhana zao.

Lwaitama (1995) akitumia kigezo cha nadharia uhakiki wa lugha alichunguza mtindo wa Rais Nyerere na Rais Mwinyi wakati wa hotuba zao. Alichunguza nomino, vitenzi, mwingiliano wa sintaksia katika hotuba za marais hawa. Utafiti huu utashughulikia uwezo wa lugha wa viongozi katika vyama mbalimbali nchini. Lwaitama alitafiti nchini Tanzania ilhali utafiti huu ni wa Kenya.

Bloomaert (1990) alitafiti kuhusu Matini za kisiasa za lugha ya Kiswahili. Alichunguza hotuba za Nyerere zinavyodhihirisha mwingiliano wa mtindo wa utamaduni na pia wa kimagharibi. Tofauti na utafiti huu ni kuwa hautaangazia mtindo.

Msanjila (1989) alifanya utafiti ambapo alichunguza sheria za hotuba rasmi nchini Tanzania. Baada ya uhuru aligundua kuwa mtindo wa kuitwa kicheo ulikuwa na majina kama mheshimiwa, mtukufu, bwana, bibi miongoni mwa hadhi zingine. Hayo yote yalibadilishwa na kuwa ndugu, msingi wa ujamaa wa Tanzania uliomaanisha, sahibu.

Haugerud na Njogu (1991) walitafiti kuhusu mikutano ya kisiasa nchini Kenya. Nao walishikilia kuwa lugha ya kisiasa ilitumiwa na wanasiasa kama mbinu ya kuelezea

ujumbe wao kwa njia tofauti ili kuwanufaisha wao wenyewe (wanasiasa) na malengo ya taifa. Utafiti huu utapiga hatua kwa kuangalia vile itikadi za mwanasiasa zinamwezesha kupata mamlaka.

Njue (1989) alichunguza mbinu zilizotumiwa kuwasilisha ujumbe katika lahaja ya Kimvita, maongezi yasio rasmi. Yahya Othman (1994) alitafiti kuhusu dhana ya adabu kwa jamii ya Waswahili Kisiwani Unguja. Mtu anahitaji kuelewa jinsi ya kufurahia au kukasirika kwa mzungumzaji na msikilizaji bali pia mtu wa tatu anayehusika. Mbinu tofauti hutumiwa kama vile kunyamaza, kubadilisha mada na kupiga vijembe. Utafiti wa Njue na Othman uliangalia lahaja za mwambao wa Pwani, ilhali utafiti wetu uliangalia lugha mahsusi iliyotumiwa na watu fulani ambao ni wanasiasa.

Michira (1993) alichunguza lugha iliyotumiwa na wachuuzi sokoni Gikomba na matangazo ya biashara ya Kiswahili katika shirika la utangazaji la Kenya -*KBC*. Habwe (1999) katika tasnifu yake ya Uzamifu alitalii kuhusu lugha ya kisiasa nchini Kenya. Iliangazia matatizo ya mshikamano, muwala na maana kipragmatiki katika baadhi ya matini ya hotuba za kisiasa katika lugha ya Kiswahili. Alitumia nadharia ya Halliday na Hassan (1976), mtazamo wa nadharia mada na kiunzi ya Brown na Yule (1983) na nadharia ya kuashiria na Grice (1975). Tofauti na utafiti huu ni kuhusu nadharia ambapo Habwe aliorodhesha misingi saba ya matini ya kisiasa kuwa na mshikamano na muwala . Utafiti huu umeangalia matini za kisiasa na jinsi

huweza kutumiwa na wanasiasa ili kupata mamlaka. Mamlaka haya hutokana na itikadi walizo nazo wanasiasa.

## 1.6 Mbinu Za Utafiti

Utafiti mdogo wa hapo awali ndio msingi wa utafiti uliofanywa. Katika ukusanyaji wa data, utafiti huu ulizingatia maktaba na mashirika ya utangazaji kama vile Shirika la Utangazaji la Kenya na Shirika la Televisheni la Nation. Katika maktaba tulisoma magazeti ambapo tuliangalia hotuba za kisiasa za mwaka 2002 hadi hivi sasa. Maktabani tuliangalia vitabu na majarida, tahakiki na maandishi yoyote yaliyohusu kazi hii ili kuendeleza hoja hizi. Maktabani tulipata maelezo kuhusu nadharia zilizoongoza utafiti huu na katika mashirika ya habari tulitazama kanda za video kuhusu hotuba za siasa.

Tulitumia sampuli isiyo yakini nayo ni sampuli kusudio ili kuwasilisha data. Wanasiasa waliochaguliwa ni wale walio na msisimko mkubwa wanaponena na kutumia lugha ya mnato katika mazungumzo yao; hivyo kusisimua hadhira. Mikoa yote nchini iliwakilishwa.

Wanasiasa waliochaguliwa ni wale waliowakilisha matapo ya NAK, LDP na KANU kwa sababu serikali iliyoundwa ni ya mseto. Pia wanasiasa waliokuwa na umahiri wa kutumia lugha ya mnato ili kuwasilisha ujumbe na maudhui yao. Lugha yao

ilivutia kwa sababu ilirembeshwa sana. Wanasiasa waliochaguliwa katika utafiti huu ni wafuatao;

| MKOA | MWANASIASA |
|---|---|
| Nairobi | Raila Odinga, David Mwenje, Reuben Ndolo |
| Kati | Joseph Kamotho, Mwai Kibaki, Uhuru Kenyatta |
| Bonde la ufa | Koigi Wamwere, Daniel Moi, Christopher Kirwa |
| Kaskazini mashariki | Bonaya Godana, Billow Kerrow, Mohammed Khalif |
| Magharibi | Kijana Wamalwa, Mukhisa Kituyi, Musikari Kombo |
| Nyanza | Otieno Kajwang', Joab Omino, Kennedy Nyagudi |
| Mashariki | Kalembe Ndile, Charity Ngilu, Kalonzo Musyoka |
| Pwani | Buya Mungatana, Sharrif Nassir, Najib Balala |

### 1.7 Upeo Wa Utafiti

Katika utafiti huu tumetazama hotuba za wanasiasa zilizowavutia wasikilizaji wengi na kuzua hisia tofauti kwa wasikilizaji. Mambo na hisia hizi zinatokana na uchanganuzi wa matini. Wanasiasa waliochaguliwa wanawakilisha sehemu mbali mbali za nchi ya Kenya.

Hotuba hizi ni za kuanzia mwaka wa 2002 ambapo wakati huu siasa nchini Kenya ilikuwa imechacha kwa vile Rais Moi alikuwa ashatangaza kuwa hatawania uongozi

wa nchi na kwa hivyo Kenya ilitarajiwa kuchagua rais mpya ili kuchukua hatamu ya uongozi baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2002.

## 1.8 Uchanganuzi Wa Data

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia namna wanasiasa walivyotumia lugha wakati wa uchaguzi wa mwaka wa 2002 hadi mwaka wa 2005. Ilichanganuliwa kwa kuzingatia miktadha iliyofanikisha matumizi hayo ya lugha. Kwa kuzingatia umilizi wa lugha katika kuelezea dhana za wazungumzaji. Data iliyochanganuliwa iliwasilishwa kwa njia ya kueleza.

# *SURA YA PILI*

## 2.0 LUGHA, SIASA, MAMLAKA NA ITIKADI

### 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tutaangazia mwingiliano uliopo kati ya lugha, siasa, mamlaka na itikadi, na jinsi zinavyotumiwa na wanasiasa. Ni muhimu kuangazia mwingiliano uliopo kati ya dhana hizi. Kumekuwepo na ukadiriaji uliopunguka wa umuhimu wa lugha katika uzalishaji, uendelezaji na mabadiliko ya ushirikiano wa uwezo na vile lugha inavyochangia kuongeza uwezo wa jamii kuhusu kutawala na kutawaliwa.

### 2.2 Lugha

Lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana. Todd (1987) ameeleza lugha kuwa mfumo wa ishara ambazo watu hutumia wanapowasiliana. Cook (1969) anaeleza kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu na ishara za kisarufi ambazo watu wa jamii fulani ya lugha huwasiliana na kupokeza utamaduni wao.

Kwa mujibu wa Ferdinand de Saussure (1916), lugha imo katika migao mitatu ambayo ni *langage*, *langue* na *parole*. *Langage* inarejelea lugha katika ujumla wake yaani ni sifa zinazoitambulisha lugha kama amali ya binadamu. *Langue* ni mfumo wa sheria za matumizi ya lugha mahsusi. *Parole* nayo ni matumizi ya mfumo wa lugha katika muktadha mahsusi. Katika ufafanuzi huu, inadhihirika kuwa lugha ni chombo cha mwanadamu.

Lugha husaidia kuweka misingi ya itikadi na mielekeo ili kudumu kwa wanasiasa na pia jamii kuimarika. Inatupasa kuelewa kuwa lugha ni mkondo ambao ni changamano. Ina vitengo vingi ndani yake. Vitengo hivi hutokana na hali kuwa lugha hutumiwa kwa njia tofauti tofauti katika mahali tofauti, miktadha tofauti, na watu tofauti. Hata kama lugha ni ile ile, tofauti yaweza kutokana na mambo kama vile umri, cheo, elimu na uwezo wa kiuchumi. Lugha vile vile huwa tofauti kutegemea utendakazi wake. Kutokana na utendakazi huu, tuna lugha ya siasa inayotumiwa na wanasiasa kudhihirisha ubunifu na unyumbufu, na lugha ina sifa bia.

Davy na Crystal (1969) wanaeleza kwamba lugha katika sekta mbalimbali za kutenda kazi huibua mitindo ya kipekee. Ni katika mgao huu tunapata lugha ya *kisiasa. Utumizi muafaka wa lugha huweza kumtofautisha mwanasiasa bora na* mbaya. Ni umahiri wa lugha ndio uliomfanya Martin Luther King kufahamika kama mtetezi wa haki za binadamu ulimwenguni. Kwa hivyo ni vigumu kuzungumzia siasa bila kutaja lugha inavyotumiwa na wanasiasa. Wanasiasa hutumia mbinu tofauti za lugha ili kuwasilisha dhana zao. Kulingana na Austin (1975) Kigezo muhimu cha lugha kama chombo kitumiwacho kufanya kitendo fulani kwa kutumia maneno kama vile kuonya, kuuliza, kulazimisha kushawishi, kukejeli, kusuta, kuaibisha na kutia au kuvunja moyo. Mwanasiasa hutumia lugha kwa muktadha anaojipata. Kuna lugha ya siasa ambayo hutumiwa na wanasiasa ili kuwasilisha hoja zao.

Lugha hutumiwa na wanasiasa kwa ajili ya kuelezea misimamo yao ili wapate mamlaka na hali ya asili na dhima ya lugha haiwezi kutenganishwa na jamii kwa jumla. Lugha huwasilisha uwezo wa watu kuweza kujumuika na jamii husika na hivyo kuelewa utamaduni wa jamii hiyo husika.

Lafall (1966:87), alielezea kuwa:

> Hali ya lugha humwelekeza mtu kwa sampuli ya utamaduni. Ni kigezo cha kumfanya mtu kujitambulisha na utamaduni fulani.

Lugha pia humwezesha binadamu kuchunguza tabia zake za kipekee na hivyo kujisemeza kinachomtofautisha na watu wengine. Mtu hupata maendeleo na lugha haiwezi kutenganishwa na mazingira. Ili mtu aweze kuwasilisha mawazo yake mwafaka ni lazima aeleze kwa kutumia lugha. Lugha huwa kama msingi wa mawazo ya binadamu. Lugha inaweza kueleweka kuwa huongoza kwa mtazamo wa mwelekeo wa utamaduni na siasa za nchi kwa jumla. Lugha na hisia za kisiasa huenda sambamba ambapo huathiri mtu binafsi na mtazamo wake kwa mazingira.

Karl Marx na Fredrick Engels (1968:116) wanasema;

> Lugha na fahamu zina umri sawa, Lugha ni fahamu iliyo ya ukweli na dhahiri kabisa. Kwa hivyo kama ilivyo lugha, ufahamu hujitokeza pale palipo na haja, ili kuwasiliana na watu wengine. Kule kutambua umuhimu wa akili tambuzi huhitaji ustadi maalum wa matamanio ya kisiasa.
> (Tafsiri yetu)

Kwa kutumia lugha, wanasiasa hunyang'anyana uwezo na mamlaka baina yao na vile vile hunyakua mamlaka hayo kutoka kwa watu na huiweka katika muungano wa ukiritimba wa uongozi pale watu wachache huhusika. Wanasiasa wana njia tofauti za kutumia lugha bila wao kutaja wazi na hivyo huweza kuhimili maongezi ya kisiasa.

Ili kudhihirisha umuhimu wa lugha Obeng na Hartford (2002: utangulizi) walisema,

> Kutumia lugha kunaweza kuunganisha mataifa yanayozozana na kuleta amani bila kuwepo vita. Hata mataifa yakiwa vitani lugha hutumiwa kusitisha vita hivyo. Kwa hivyo lugha inaweza kuanzisha vita na pia kuleta amani. Lugha hutumiwa kujenga au kubomoa wapinzani. Ili kuimarika kisiasa lugha huwa muhimu. Lugha hutumiwa ili kuhimiza au kuwakatiza wananchi wasiandamane. Lugha husaidia kujenga msimamo wa mtu. Lugha pia husaidia kuweka misingi ya itikadi na mielekeo ili kumdumisha mwanasiasa na jamii kwa jumla. Mwanasiasa hutumia lugha ili kufanya sheria na umuhimu wa lugha ni kuwa husaidia uzalishaji mali, hurekebisha na pia hubadilisha mawasiliano ya kijamii ili kupata mamlaka. Lugha husaidia kuzua urasimu katika fahamu ambapo watu wanaotawaliwa huweza kujua umuhimu wa kujikomboa. Kila taaluma ina lugha yake mahsusi. Usione haya kutumia lugha kwa manufaa yako mwenyewe kwani Mungu hakuuza lugha wala hekima. Hakuna aliye na uhodhi kwa lugha wala hekima.
> ( Tafsiri yetu)

Ni muhimu kutaja kuwa wanasiasa wana lugha yao ambayo imezindua hisia za kiusomi. Ni vigumu kuongea kuhusu siasa bila kutaja lugha kwa sababu siasa

huendelezwa kupitia kwa lugha. Obeng (2002) alieleza kuwa uwezo wa mwanasiasa wa kuhutubu humfanya kuwa na wadhifa na mamlaka kwa vile anawakilisha uwezo wa kisiasa. Upo msemo wa Kiyoruba unaosema kuwa maongezi ni kama yai, liangukapo huvunjika. Hii ina maana kuwa matumizi ya lugha vibaya inaweza kuleta madhara katika maongezi.

Talleyrand (1969: 54) alielezea amali ya lugha;

> kama lugha, mtu anaweza kufanya mambo mengi na upanga lakini hawezi kuikalia. Kwa hivyo lugha huweza kufanya matendo mengi katika hali ya kisiasa na wanasiasa huitumia kwa manufaa yao wenyewe.

Mwanasiasa anaweza kuelezea matatizo yaliyoko katika jamii kwa kutumia lugha na pia huweza kuelezea itikadi anazoziamini. Fairclough (1989:112), katika *The power of Language* alielezea uhusiano wa lugha;

> Lugha ni mchakato tendani wa jamii hasa tukizingatia sana tofauti ya mazungumzo na matini. Matini ni zao lakini mazungumzo ni mfumo wote wa mawasiliano. Kuna njia za kungamua lugha ambazo zimejikita katika akili. Njia hizo pia ni za kijamii kwa sababu mianzo na asili zake ni katika jamii na hutegemea mahusiano ya jamii. Watu huweza kuhifadhi ndani ya akili kile ambacho kimezalishwa na jamii na hukitoa katika mahusiano ya kijamii. Mahusiano huhusishwa katika mahusiano ya kiutamaduni. Mazungumzo ndiyo yanatoa nguvu zinazoelekeza maisha ya jamii kwa mfano mbinu tofauti za kiakili hutumika wakati mtu anaposoma shairi kwa upande mmoja na wakati anaposoma gazeti kwa upande mwingine. Mazungumzo huhusisha masharti ya jamii ya uzalishaji na uchambuzi au ufasiri, masharti ambayo yanahusiana katika viwango vya jamii.(Tafsiri yetu)

Hali ya kuelezea kuhusu mamlaka na uwezo wa mwanasiasa au msanii yeyote kufasiri itikadi aliyo nayo yote haya huelezwa kupitia mazungumzo. Njia mbili za wale wenye nguvu wanazoweza kutumia ni kushurutisha na kulazimisha. Mbinu mbalimbali hutumiwa na serikali ili kusuluhisha matatizo na kuelezea sera ili wananchi wakubali utawala. Mwanasiasa anaweza kueleza sera za nchi kwa kutumia lugha.

Mazungumzo hivyo huhusisha masharti ya jamii kama vile ya uzalishaji na *uchambuzi au kufasiri masharti hayo yanayohusiana katika viwango tofauti vya* jamii. Masharti haya matatu ya jamii hujenga jinsi watu huzalisha na kufasiri na ndiyo inayoeleza jinsi mazungumzo huzalishwa na kufasiriwa. Kunazo aina muhimu za mazungumzo ambazo hujumuisha itikadi na ambazo huhalalisha mahusiano ya kijamii na hujitokeza katika jamii ya kisasa kiasi kwamba zimeathiri nyanja kubwa ya mazugumzo. Maongezi kuendeleza itikadi, na hivyo basi kwa kuongozwa kwa kukubali habari za kila siku huweza kuamuru jamii lakini kuongezeka kwa kutegemea kuamuru huko kwa hiari ndicho chanzo cha sura nyingine bora ya mazungumzo ya kisasa. Mwelekeo wa mazungumzo yanayoongoza jamii kuelekea usawa ulioigizwa na kutolewa kwa alama za kijuujuu za nguvu na mamlaka. Hii hupatikana katika matini, mazungumzo, matangazo, elimu na serikali.

Uhusiano wa mazungumzo na miundo ya jamii ni ya kipembuzi na huathiri mifumo ya jamii na huchangia mabadiliko katika jamii na kwa sababu hiyo mazungumzo

huchukua nguvu nyingi katika mahusiano ya mamlaka na migogoro ya uwezo. Uwezo wa serikali huthibiti mpango wa mazungumzo huelekeza kudhibiti mamlaka, nguvu na uwezo. Uhusiano wa uwezo/nguvu/mamlaka na mazungumzo ni uwezo katika mazungumzo yenyewe. Mazungumzo ndicho chombo kinachowezesha mahusiano ya mamlaka/nguvu, uwezo kufanyika na kuigizwa. Migogoro juu ya lugha inaweza kujitokeza kama migogoro ya itikadi pevu za aina ya mazungumzo, kwa mfano, katika siasa kila chama cha kisiasa hujaribu kushinda wafuasi kwa kutumia mazungumzo au maandishi fulani na ambayo chama hicho huchukulia ndiyo ya asilia zaidi kuliko ya vyama vingine.

## 2.3 Uhusiano wa mamlaka na lugha

Kumekuwepo na kutoelewa kuhusu umuhimu wa lugha katika uimarikaji, uendelezaji na mabadiliko ya ushirikiano wa mamlaka na vile lugha inavyochangia kuongeza mamlaka ya jamii kuhusu kutawala au kutawaliwa na wengine. Kwanza ni vizuri kuelewa kuwa lugha ni sehemu ya jamii na pili, lugha ni michakato ya jamii na tatu, lugha ni michakato inayotawaliwa na jamii, utawala ambao unatokana na maswala mengine yasiyohusiana na lugha .

Kimsingi, uhusiano wa ndani uliopo kati ya lugha na jamii ni kuwa lugha ni sehemu ya jamii. Matukio ya lugha ni matukio ya kijamii, na kinyume chake. Matukio ya lugha ni ya kijamii kwa maana wakati wowote watu wanapozungumza, kusikiliza, kusoma au kuandika, wanafanya hivyo kwa njia ambazo zimebainishwa na jamii na ambazo zina athari katika jamii. Matukio ya jamii nayo ni matukio ya lugha kwa

vile lugha inavyokuwa katika muktadha wa jamii sio tu mfuatano bali pia ni mazoea kwa mfano katika migogoro kuhusu maana ya misamiati ya kisiasa wakati mwingine watu hubishana kuhusu maana ya maneno kama vile demokrasia, utaifishaji ubepari na kadhalika. Mara nyingi wao hutumia maneno kwa njia tofauti tofauti na mifano mizuri ni rahisi kupatikana katika malumbano au mabishano kati ya viongozi wa vyama vya kisiasa, au mataifa. Wakati mwingine malumbano hayo huonekana kama tu mianzo ya matokeo ya mazoezi ya kisiasa. Lakini hizi ndizo siasa kamili. Siasa kwa kiwango, huwa katika mabishano, majadiliano na mashindano na mapambano yanayotokea katika lugha au juu ya lugha. Lakini sio kwa sababu ya uhusiano linganifu uliopo kati ya lugha na jamii kama sehemu mbili za kitu kimoja. Bali zote ni jamii, na lugha ni ncha ya jamii. Matukio yote ya kijamii si lugha lakini yote huwa na misingi au asili katika lugha.

## 2.4 Lugha ya siasa

Katika matini za kisiasa, kwa jumla muktadha hujumuisha madhumuni, lengo na utendaji kazi wa matini hayo, wahusika wanaosikiliza, mada ya pahali matini hiyo inafanyiwa. Mawasiliano ya kisiasa hutawala katika hotuba za Rais, majadiliano ya Bunge, mikutano ya kisiasa, propaganda na wakati mwingi, katika shughuli za kijamii kama vile mazishi, ndoa, misa na tohara. Reeves (1983) anasema kuwa sura muhimu katika muktadha wa matini za kisiasa huhusisha nafasi katika jamii na matendo ya wahusika katika siasa.

## 2.5 Siasa

Siasa inajihusisha na mitafaruku ya kijumla na njia za kusuluhisha mizozo hiyo. Mizozo huzuka kwa ajili ya sababu zisizoweza kuepukwa katika maisha ya binadamu. Mizozo katika jamii hutokea kwa sababu zifuatazo: kwanza, upungufu wa rasilmali, ili watu waendelee kuishi watu hubadilisha rasilmali kwa vitu wanavyohitaji. Lakini matarajio ya watu huwa mengi kuliko rasilmali zinazopatikana, au wakati mwingine matarajio ya kikundi fulani yanaweza kuwa pingamizi kwa kikundi kingine. Hii husababisha msingi wa pili wa mitafaruku ambayo, ni thamani na nia yao. Kwa hivyo tofauti katika mawazo, mitazamo, makabila, dini na utamaduni inaweza kuleta mitafaruku katika jamii. Mikinzano pia inaweza kuhusu hali ya afya ambapo kundi moja linaweza kutetea matibabu bila malipo ilhali lingine lizungumzie kuhusu malipo ili kunufaisha mashirika ya afya ya kibinafsi. Kwa hivyo siasa inahusu mitafaruku na jinsi wanasiasa wanavyojaribu kusuluhisha mitafaruku iliyoorodheshwa hapo juu.

Raila anaposema ,

> I am not going to talk to you about Obama. Best representation is like a bikini suit. But since I cannot wear it, I am not going to talk about it in my speech. The French say a Kiss without Moustache is like soup without salt. So without a little bit of politics...

> Sitazungumzia kuhusu Obama. Kuwakilishwa kuzuri ni kama suti ya bikini; kwa vile sijui kuivaa sitaweza kuzungumzia katika hotuba yangu. Wafaranza hunena kuwa busu bila masharubu ni kama mchuzi bila chumvi. Kwa hivyo bila kuongea kuhusu siasa ni kama mchuzi bila chumvi. (Tafsiri yetu).

Siasa inalinganishwa na chumvi inayowekwa kwa mchuzi ili mchuzi ule upate utamu. Kwa hivyo siasa huathiri maisha ya kila mtu.

Watoto wawili katika shule ya chekechea wanapozozana kuhusu nani atakayechezea mwanaserere huhitaji suluhisho la kisiasa. Kuna tatizo na kuna haja ya kupata utatuzi. Watoto hao wanaweza kupigana na yule atakayeshinda kunyakua mwanaserere au mwalimu kuingilia kati ili kupata suluhu kati ya watoto hao wawili. Hivyo kama ilivyo kwa mwalimu kupata suluhisho, siasa pia huwa na mitafaruku ambayo suluhu huhitajika.

## 2.6 Itikadi

Kulingana na Musokile (1993) itikadi ni mawazo fulani ambayo ni msingi wa nadharia ya mfumo wa kisiasa au uchumi. Pili ni imani katika jambo fulani kwa mfano dini, jinsi ya mapokezi yake, wanavyofuata jambo fulani, fikira za kuaminika. Mwandishi yeyote wa fasihi huongozwa na itikadi maalum. Kama ilivyo kuwa mwandishi huongozwa na itikadi, wanasiasa pia nao huongozwa na itikadi. Kulingana na Mohammed (2001), Itikadi ni mawazo makuu yanayotawala mtazamo wa mwandishi kuhusiana na maisha kwa jumla na jinsi mawazo haya yanavyotusaidia au kukwamisha juhudi zetu za kutatua matatizo ya ulimwengu. Ujenzi wa jamii mpya unadhihirika katika hotuba ya Marehemu Wamalwa Kijana katika Hoteli ya Hilton, Nairobi tarehe 22/10/2002;

For me, we are today writing Kenyan history in golden letters The realization by those of us in the opposition that the way to free our country from tremendous poverty and total collapse from all institutions including economic, civil, judicial and in every other way is for us to come together as wise people to work and fight together to remove this government from power. I am justified in the book am writing that Nyayo era was a great error. Ladies and gentlemen we in opposition must do everything for the children of Kenya and not for ourselves anymore. Opposition unity is only a reality if we can do everything recognizes and accepts one principle. Alot of our children have not offended anybody yet we are destroying their future. If a person is going to subject them to further suffering then a way should be found of getting rid of me. We can only succeed if we leaders can renounce our own personal ambition and resounding that we will do everything for the children of Kenya.

Leo, tunaiandika historia ya Kenya upya kwa herufi za dhahabu. Kufahamu kwetu wale walioko katika upinzani kwamba ili kuiweka nchi yetu huru kutoka kwa umaskini usio kifani na maanguko makuu ya kiuchumi, kijamii, kisheria na njia nyinginezo zote, lazima tuungane kama watu werevu na tufanye kazi pamoja, tupigane pamoja ili kutoa serikali hii ya (KANU) mamlakani. Nina ukweli katika kitabu ninachoandika kuwa enzi ya nyayo ilikuwa makosa makuu. Mabibi na mabwana, sisi katika upinzani lazima tuwafanyie vyovyote watoto wa Kenya bali sio kwetu mtakuwa dhahiri tu, iwapo tutakubali msimamo mmoja. Kwamba watoto wetu hawajamkosea yeyote, ilhali tunawaharibia maisha yao ya baadaye. Iwapo yeyote atazidi kuwanyanyasa hata ikiwa ni mimi basi njia ya kunimaliza inapaswa kutafutwa. Tutaweza tu kufaulu iwapo sisi viongozi tutaweza kutupilia mbali ubinafsi na kusema kuwa tutafanya kila kitu kwa sababu ya watoto wa Kenya...(Tafsiri yetu)

Kile Wamalwa alichokuwa akiangazia ni umoja wa vyama vya upinzani ili kuweza kuking'oa chama cha KANU mamlakani. Wamalwa aliangazia umoja ili kujenga jamii mpya isiokuwa na ufisadi, wizi, mauaji na umaskini. Kwa ajili ya shinikizo iliyokuwepo na maneno yaliyotumiwa na wanasiasa vyama, vya upinzani viliweza kuungana na kutoa mgombeaji wa urais mmoja aliyeweza kushinda uchaguzi mkuu.

Raila anaposema,.

> *If you are a polygamous you must love all. Otherwise you create a situation you cannot handle. When you show your love to only a section of your people, there in lies the problems as chaotic situations are inevitable.*
>
> Iikiwa umeoa wanawake wengi yafaa uwapende wote, la sivyo utasababisha mitafaruku usiyoweza kuitatua.(Tafsiri yetu)

Kulingana na usemi wa hapo juu inadhihirika wazi kuwa hii ni jamii inaruhusu mwanadamu kuwa na wake wengi. Pili, inadhihirika wazi kuwa mwanasiasa huyu alikuwa akizungumzia matatizo katika serikali ya NARC ambapo Rais wa nchi alichagua watu wengi kutoka tapo la NAK na wachache kutoka LDP ambapo wale wa LDP walikuwa wakinung'unika. Pia kazi za serikali zilipewa watu kutoka jamii moja na kuacha makabila mengine.

Kuhusu itikadi ni hali ya kusadiki au kuchukulia kuwa ni kweli ambapo wananchi huchukulia kama kweli mawazo wanaoambiwa na wanasiasa. Fairclough (1994) anatoa mfano ufuatao: Daktari anajua kuhusu dawa ya kutibu mgonjwa. Daktari anajua kuzorota kwa siha ya mgonjwa, mbinu za kutibu, ingawaje mgonjwa hajui mbinu hizi. Kwa hivyo daktari hufanya maamuzi na hudhibiti mazungumzo na

mgonjwa na utabibu na hivyo mgonjwa hufuata na kushirikiana na daktari ili atibiwe. Kwa hivyo lugha hutumiwa baina ya watu wawili na kule kusadiki ndicho kigezo muhimu cha mtu kupata matitabu.

## 2.7 Lugha na itikadi

Uhusiano uliopo kati ya lugha na jamii ni mkubwa kwa sababu bila lugha hakuna jamii na pia bila jamii hakutakuwa na lugha. Lugha ndicho kitambulisho cha jamii. Mawasiliano kwa kutumia lugha huhusisha mazungumzo na matini. Kwa mujibu wa Fairclough katika *Language and power* (1987) kuna uhusiano wa ndani kati ya lugha na jamii. Wakati wowote watu wanapozungumza, kusikiliza au kuandika wanafanya hivyo kwa kutumia lugha. Mbinu zinazowezesha watu kuwasiliana zimebainishwa na jamii. Wanasiasa hutumia lugha ili kuwasilisha hoja zao kwa umma na mambo yote yanayohusiana na mawasiliano huhifadhiwa katika akili na yanapotolewa hutolewa kulingana na matukio ya jamii.

## 2.8 Mamlaka

Ili kusuluhisha mitafaruku mamlaka hutumiwa na wanasiasa. Mamlaka hudhihirika pale ambapo kuna mikinzano. Mamlaka ni uwezo wa mtu au watu fulani wa kumiliki na kuthibiti tabia na maisha ya wengine. Uhusiano huu wa mthibiti hauwezi kubadilishana yaani wote hawawezi kuwa na nguvu za namna moja kwa wakati mmoja. Dhana hii ya nguvu ndio msingi katika hali ya kutokuwa na usawa katika jamii. Mamlaka hukifanya kikundi fulani cha watu kufanya watakavyo licha

ya pingamizi kutoka kwa wale wengine. Udhibiti huu waweza kuwa katika matendo au akili kwa mfano kikundi chenye mamlaka kama vile wanasiasa chaweza kuthibiti akili zao.

Mfano wa matumizi ya matendo ni pale polisi wanapotumia nguvu kuzima maandamano au fujo za watu. Udhibitishaji kwa kuathiri akili za watu na ambao ni mbinu inayofaulu sana hufikiwa kupitia ushawishaji, utumiaji wa hila kama vile wanasiasa wanavyotumia lugha ili kubadilisha mawazo ya wengine yapate kuafikiana na mahitaji ya kundi tawala. Hapa ndipo nadharia ya usemi hakiki huafikiana kwani kule kuongoza mawazo ya wengine ni kazi ya matini (iliyosemwa na kuandikwa). Huku kuongoza mawazo ya wengine huendeshwa kwa njia inayoonekana kama kawaida na hata kubalifu. Nadharia hii huafikia uwezo wa lugha kwa vile huchunguza mikakati ya usemi ambayo hufanya kuonekana kawaida ile hali ya kijamii inayohusiana na kutokuwepo kwa usawa.

Mara nyingi wenye mamlaka kama wanasiasa hutumia vibaya mamlaka yao kama vile kukiuka kanuni za demokrasia, haki ya wanawake, watu weusi, watu maskini, wasiofahamu sheria. Mamlaka na utawala ni mambo ambayo huwa yamepangiwa na kufanyiwa asasi. Asasi hizi huungwa mkono na washiriki wake, kuidhinishwa na korti, kuhalalishwa na sheria kama vile miswada ya bunge ambayo huwasilishwa na wanasiasa. Iwapo akili za watu zaweza kutawaliwa kiasi cha wao kukubali

utawala huo na kutenda kulingana na matakwa yao wenyewe kulazimishwa. Hali hii inaitwa hejemonia yaani utawala ambao una kibali cha watawaliwa.

Mpangilio huu wa nguvu na mamlaka pia huwa na mfumo wa ngazi hivi kwamba baadhi ya washiriki wana majukumu maalum katika upangaji, utoaji wa maoni na kudhibiti shughuli za uongozi. Hawa ndio wana uwezo fulani kwa kufikia usemi ambapo Bourdie Pierre aliita mamlaka ya ishara ambapo wanasiasa huchagua lugha wanayoitumia ili kudumisha mamlaka yao; na alitamka hivi aliponukuliwa na Fairclough katika The Power of Language,(1987:215)

> Mawasiliano ya kiisimu baina ya wazungumzaji hutegemea uhusiano wa kijamii uliopo baina ya wazungumzaji. Watu huchagua lugha ambayo ina hadhi fulani kutegemea muktadha wa matumizi. Watu huhitaji kutumia lugha yenye hadhi kuu. Hata hivyo nafasi ya kujifunza lugha yenye hadhi kuu ya zote ni nadra zaidi katika jamii na nafasi hizo vile vile hazijagawanywa sawa.

Kuna uhusiano kati ya wenye mamlaka katika jamii na ufikiaji wa usemi. Wenye mamlaka ndio wana uwezo wa kutumia tanzu tofauti za usemi. Wanaweza kuthibiti miktadha mbalimbali, washiriki, hadhira, upeo na vipengele au sifa ya matini. Watu wa hali ya chini huenda wakawa na usemi tu baina yao na jamaa zao tu, marafiki au wenzi wao wa kikazi.

Kwa kurejelea kanuni ya maafikiano ya Scotton (1993), katika mazungumzo mtu huchagua lugha ambayo italenga mahitaji yake ambayo anataka yashughulikiwe

katika muktadha huo wa mazungumzo. Utaona kuwa lile tabaka aali kama wanasiasa lenye uwezo wa kufikia uneni basi litaendeleza utabaka katika jamii kwa kupitia matini. Kwa hivyo matini au hotuba hutolewa maelezo, ufafanuzi na kuhakiki namna ambavyo matini za kiutawala zinavyoathiri mielekeo na itikadi za jamii. Hivyo huchunguza miundo ya matini na kuona vipi mzungumzaji mwenye mamlaka anavyohalalisha nguvu na jinsi hadhira ilivyojiitikia.

Hatua hii huonyesha jinsi uneni unavyoathiriwa na miundo ya jamii. Hapa tunajiuliza ni kwa namna gani mazungumzo hutokana na miundo ya jamii na ni kwa namna gani mazungumzo hayo hudumisha au kukosoa uhusiano unaotarajiwa kuwepo katika jamii kwa jumla.

Kwamba lugha ni mfanyiko tendani wa jamii hasa kule kuangalia kile kinachotofautisha mazungumzo na matini. Matini ni zao lakini mazungumzo ni mfumo wote wa mawasiliano. Matini huhusisha uzalishaji ambapo matini ndilo zao. Kuna njia za kung'amua lugha ambazo zimejikita kwenye akili na kwa hivyo ni njia tambuzi kwa ambavyo zimo akilini, lakini pia ni za kijamii kwa vile zina mianzo yake katika jamii na asili yake na imetokana na jamii na hutegemea mahusiano ya jamii. Watu huweza kuhifadhi ndani ya akili kile ambacho kimezalishwa na jamii na hukitoa katika matukio ya kijamii, ikiwemo mazungumzo. Hili ndilo hutoa nguvu zinazo chonga jamii uhai. Na sio asili ya rasilmali za akili, lakini pia masharti ya

kuzitumia. Kwa mfano mbinu tofauti za kiakili zinatarajiwa wakati mtu anaposema shairi kwa upande mmoja au (na) kusoma tangazo gazetini upande mwingine.

Mazungumzo au matini na utaratibu au mpango wa mazungumzo imetumiwa na Michel Foucault (1997). Neno mazungumzo na mazoea yana kile tunachoweza kukiita utata teule. Yote yanaweza kutaja au kusema kile watu wanachokifanya katika wasaa fulani ama vile watu hufanya katika tukio fulani.

Nguvu za itikadi na uwezo wa kupanga, mazoea kama maarifa ya kawaida ni muhimu katika ukuaji wa nguvu za kiuchumi na kisiasa. Yote haya yamefanywa kupitia mazungumzo. Njia mbili za wale wenye nguvu wanazoweza kutumia ni kushurutisha na kulazimisha. Mbinu mbalimbali hutumiwa na serikali kuwafanya wakubali utawala wake. Itikadi ndiyo chombo mwafaka cha kuafikia hayo.
Kunazo aina muhimu za mazungumzo ambazo hujumuisha itikadi na ambazo huhalalisha mahusiano ya kijamii na ambazo hujitokeza katika jamii ya kisasa kiasi kwamba zimewakolini nyanja kubwa ya mazugumzo. Mazungumzo ni kigezo mwafaka cha kuendeleza itikadi. Hivyo basi kwa kuongozwa kwa kukubali, kwa mfano habari za kila siku huweza kuamuru jamii lakini kuongezeka kwa kutegemea kuamuru huko kwa hiari, ndicho chanzo cha sura nyingine zenye ubora wa mazungumzo ya kisasa. Mwelekeo wa mazungumzo yanayoongoza jamii kuelekea usawa ulioigizwa na kutolewa kwa alama za kijuujuu za nguvu na mamlaka. Hii hupatikana katika matini ya mazungumzo, matangazo, elimu na serikali.

Uhusiano wa mazungumzo na miundo ya jamii ni ya kipembuzi na huathiri mifumo ya jamii na huchangia mabadiliko katika jamii kwa sababu ya hayo mazungumzo huchukua nguvu nyingi katika mahusiano ya uwezo, nguvu na migogoro ya uwezo. Uwezo wa serikali (wenye nguvu) huthibiti mpango wa mazungumzo ni kudhibiti mamlaka, nguvu na uwezo. Uhusiano wa uwezo/nguvu/mamlaka na mazungumzo ni uwezo katika mazungumzo yenyewe na uwezo wa mazungumzo yenyewe ndicho chombo kinachowezesha mahusiano ya mamlaka/nguvu,uwezo kufanyika na kuigizwa. Mazungumzo tawala na tawaliwa, migogoro juu ya lugha inaweza kujitokeza kama migogoro ya itikadi pevu za aina ya mazungumzo. Kwa mfano katika siasa kila chama cha kisiasa hujaribu kushinda wafuasi kwa kutumia mazungumzo au maandishi fulani na ambayo chama hicho huchukulia ndiyo ya asilia zaidi kuliko ya vyama vingine.

## 2.9 Hitimisho

Lugha inahusu majadiliano ya mamlaka au uwezo na uwezo wa kumudu lugha kikamilifu ni njia ya kujipatia mamlaka. Itikadi za mwanasiasa zinaweza kuwasilishwa na kwa matumizi ya lugha teule inayowatofautisha na watu wengine. Wale wanaotumia lugha kupata mamlaka ndio wenye nguvu zaidi katika mamlaka hayo. Lugha ina uwezo mkubwa kwa sababu inajenga mahusiano ya kindani kati ya wazungumzaji na hadhira yao. Lugha inawezesha wanasiasa kujiendeleza na kuhifadhi mamlaka hayo.

# *SURA YA TATU*

## 3.0 UCHANGANUZI WA DATA YA HOTUBA YA SIASA

### 3.1 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia tulijadili dhana ya lugha ya siasa, mamlaka wapatao wanasiasa kwa kutumia lugha husika na pia itikadi za wanasiasa ili kuwasilisha ujumbe wao. Kwa hivyo itikadi ya mwanasiasa ni muhimu ambapo mwanasiasa hupata mamlaka na uwezo kwa kutumia lugha muafaka katika nyanja hii ya kisiasa. Kulingana na nadharia ya uhakiki usemi ambayo huonyesha matukio ya kiusemi au maandiko na vile yanaweza kuathiri matukio katika jamii. Kwa hivyo matini ya kisiasa huathiri matukio katika jamii. Ili kuelewa usemi ni bora kuelewa maana katika matumizi yake ambapo yafaa mtu aelewe kipengee hicho kilisemwa kwa muktadha upi. Na wanasiasa huorodesha itikadi zao ili kuelezea kile wanachokusudia.

Malumbano kati ya vyama yameendelezwa kupitia kwa lugha ya tamathali za usemi. Kwa hivyo tamathali zinazotumiwa na wanasiasa katika matapo hayo mawili na taathira zake kwa wananchi na demokrasia.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), tamathali za usemi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana zingine tofauti au zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu iliyokusudiwa na mtunzi au mzungumzaji. Tamathali nzuri

huyakinisha na kuipa uhai na kuzindua akili ya msomaji au mzikilizaji na kuacha athari za kudumu katika hisia na mawazo yake.

Tamathali kulingana na Clinton na Ilyin (1993) husaidia kuelewa dhana ngumu na iliyo dhahania kwa kutumia wazo linalofahamika. Tamathali pia hufanya mambo kadha wa kadha katika matini za kisiasa kama vile kusihi, kuonyesha umoja na pia kutotaja dhana wazi.

Tamathali hutumika katika mazingira halisi ya kijamii na hazitoki katika ombwe tupu. Zinabuniwa na hutoka katika shughuli za kila siku za maisha ya wanajamii. Tamathali za usemi ni chombo cha kutolea mawazo ya jamii, chombo cha kuumbua hisia zao na kukuza ari yao ya kisiasa. Pia huelezea itikadi zao za kimaisha na jamii husika. Katika kuelezea hali mbalimbali katika mazingira ya kisiasa, wanasiasa wametumia tamathali za usemi kuhamasisha wananchi na kuonyesha namna wanavyoendelea kunyonywa, kunyanyaswa na kuonewa na viongozi wao.

Maudhui yanajitokeza wazi pale viongozi wanapotumia tamathali hizi. Tamathali za usemi zina majukumu tofauti katika matini ya kisiasa. Mojawapo ni kuelezea sera kwa kufafanua dhana. Siasa inahusu kushawishi ambapo tamathali hutumiwa sana; Kwa mfano Lakoff (1992) anabainisha vile serikali ya Bush ilitumia tamathali ili kuhalalisha vita vya Ghuba.

Tamathali hutumiwa ili kuleta umoja baina ya makundi na wakati mwingine hubagua makundi mengine. Obeng (1997) ameeleza kuwa tamathali hutumiwa ili kujiepusha kuzungumzia wazi kuhusu miiko katika jamii husika.

Tamathali hutumiwa kama kigezo cha kuelewa dhana tofauti. Usomi kuhusu tamathali husaidia kuelewa vile ukweli unavyoumbika na unavyoainishwa. Kwa hivyo tamathali zimezaana katika itikadi ya jamii husika. Baadhi ya viongozi wameona wajibu wao wa kufumbua wananchi macho ili waone ukweli kuhusu serikali waliojitoa muhanga kupigania. Lengo kuu la kutumia tamathali ni kuonyesha wananchi kuwa juhudi zao za kupiga kura hazikuwafanikisha kupata viongozi waliowatambua kwani mabadiliko katika mazingira ya kisiasa yameenda kinyume na matarajio ya wananchi. Rai hiyo imeongezeka zaidi baada ya kuingia kwa serikali ya umoja wa kitaifa ambayo imeshirikisha vyama vilivyoshindwa kwenye uchaguzi wa mwaka 2002. Baadhi ya viongozi wanaona kama usaliti kwa mwananchi ilhali wengine wanaona kama mbinu ya serikali kujidhibiti baada ya kukabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa baadhi ya wale waliounda serikali.

Kupitia kwa tamathali za usemi viongozi wanashinikiza wananchi kudai haki zao za kutawaliwa na kuongozwa na viongozi waliowachagua wala si wale waliowakataa kupitia kwa kura. Kuna aina nyingi za tamathali ambazo zimetumiwa na wanasiasa lakini tutaangalia baadhi yake. Ni kutokana na tamathali za usemi ndipo mawazo ya kiisimu huzua hisia katika ubongo wa mwanadamu.

Hotuba ya Mheshimiwa Mungatana huko Kitui wakati alipokuwa katika eneo Bunge la Mheshimiwa Ngilu, tarehe 27/3/ 2004 Mungatana alisema;

> Wakati tulikuwa tunapiga kura tulikuwa tunapiga kwa chama cha NARC. Sisi tumetoa chama kimoja kinaitwa KANU, tukaweka chama cha NARC. Sasa nimefika Nairobi nikakuta aaai mambo yamebadilika, jamaa mmoja anasema LDP. Jamaa mmoja mweusi sana- Nyang,au wewe LDP, LDP mama yako. Hawana msimamo tangu mwanzo sisi tuko ndani ya serikali kwa vile tunajua serikali hii imetufanyia nini. Afadhali KANU ina policy inasema haiwezi kusomesha watoto bure lakini LDP haina policy yoyote. Policy yao ni kufuata mtu mmoja mweusi.
>
> Wajua watu wengine hawakupata taabu kama huko kwetu wanajua serikali ni kama ile ya zamani na wanaweza kuiangusha wakati wowote.
> Watu wa LDP wakiambiwa na huyu mtu mweusi leo turuke kwa mto, wanaruka. Leo twende Mombasa wanafuata chama ambacho hakina policy hata moja. Hiyo inawezekana kufuata chama kama hicho?
> Watu: La, hatuwezi.
>
> Na mtu kama Balala pia anapingana nami nashangaa mikono hiyo nyororo inaweza kukamata mamba.
> Na ikiwa Pastor atakuchukua kuwa wewe umeokoka hawezi kukufanya siku hiyo mkuu wa kanisa au pastor mdogo kwa hivyo waokoke sawa sawa.

Tamathali huwasisimua watu wakati wanasiasa wanapozitumia, Kwa hivyo ni kifaa muhimu katika lugha ya siasa. Kwa kutumia tamathali wanasiasa huwazuga wasikilizaji ambapo wao huwashangilia na kuwaunga mkono. Kulingana na Leech (1969) anaeleza kuwa tamathali husaidia kuhamisha maana ya dhana.

Raila anafananishwa na nyang'au. Hii ni tamathali ya ufananisho ambapo nyangau ni mnyama anayejulikana kwa kujitakia mlo pekee yake bila kujali maslahi ya wengine. Raila analinganishwa hivyo na mnyama huyo kwa vile kulingana na hali yake ya kupinga serikali anaonekana kana kwamba anataka uongozi wa nchi. Raila alitaka kuwa Waziri Mkuu mwenye mamlaka yanayozidi ya Rais. Mungatana anatumia lugha ya matusi kwa kusema "LDP mama yako". Anakikejeli chama cha LDP kuwa sera yao ni kufuata tu mtu mweusi na kukikejeli chama cha KANU eti sera yao ni kuwa hakiwezi kutoa elimu ya bure. Wanachama wa LDP wanadhihakiwa na Mungatana kuwa wao hufuata tu mawazo ya Raila hata ikiwa maoni yake yatawatia mashakani kama vile kutumbukia mtoni ambapo, mto ni jazanda inayosimamia maafa.

## 3.2 Tamathali za ufananisho

Tamathali za ufananisho kama vile tashbihi, sitiari jazanda. Zimetumika kwa mapana na marefu katika kumbi za kisiasa.

> If you see a lion rained on you may think it is a cat.
>
> Ukiona simba amenyeshewa mvua, unaweza ukafikiria ni paka. (Tafsiri yetu)

Kile Raila alichokuwa akieleza ni kuwa kunyamaza kwake na wafuasi wa chama chake sio kwa uoga lakini wakichokozwa basi bila shaka watadhihirisha uwezo wao wa kujitetea.

If you see a dog barking you know it has been sent by its master not the dog, so you deal with the master not the dog or something to that effect.

Unapoona mbwa akibweka, unajua kuwa imetumwa na mwajiri wake: kwa hivyo unaafikiana na mwajiri na sio mbwa. (Tafsiri yetu)

Raila anamfananisha Mungatana na Mbwa ambaye ametumwa na mwajiri yaani watu (wanasiasa) walio na ushawishi mkubwa serikalini wanaotoka sehemu ya Mlima Kenya. Kwa hivyo Raila anaonelea hana wakati wa kujibizana na Mungatana bali atapambana na mwajiri wake. Mungatana anamufananisha Rais Kibaki na mhubiri; ilhali Raila anafananishwa na mtu aliyeokoka wakati huo. Hivyo hawezi kupewa mamlaka katika kanisa.

Kuhusu mitafaruku ya NAK walitaka LDP ijitoe katika muungano. Raila alitumia methali isemayo kuwa,"hasira za mkizi,furaha ya mvuvi".

Hapo anaonyesha kuwa wanasiasa wa NAK wanataka LDP itoke kwa muungano ndipo wanasiasa wa (NAK) wapate uwezo wa kupora mali ya wananchi kwa kuendeleza ufisadi.

Hotuba ya Koigi Wamwere kule Subukia tarehe 5/2/2005 inadhihirisha jamii ya unyanyasaji na dhuluma kwa wanyonge, na alisema yafuatayo;

Mimi namsihi namna tunapomtakia mema naye pia atutakie mema; anapoweka milioni mia moja mfukoni aturuhusu tulime mahindi. Kama tumemchinja ng'ombe na wakala mafuta kwa nini wanatukataza tusile mkia. Naye asitukataze kulima. Kama Wangari

> alikuwa akipinga nyinyi akiwa mdogo kama Wamwere na wakati huu amekuwa mkubwa kama Mandela, nguvu zake zimeongezeka mtamchezea kwa kwenda kuchukua miti kule.... mtafukuzwa!......

Inadhihirika wazi kuwa hii ni jamii iliyo na itikadi ya kuamini kuwa mtu aliye na fedha nyingi yafaa aabudiwe na kutukuzwa bila ya kujali maslahi ya wengi walio maskini. Koigi alitumia lugha chochezi ambapo baada ya siku chache serikali ilipoanza kuwatoa maskwota katika mashamba yaliyo karibu na misitu, maskwota hao walianza vita. Watu walikuwa wakikuza mimea katika misitu lakini serikali ilipiga marufuku upanzi wa mimea na hivyo kuhimiza upanzi wa miche bila kujali maskwota waliokuwa wamemiliki mashamba hayo kwa muda mrefu. Uwezo wa lugha unadhihirika ambapo koigi anaposema kwenda kuchukua miti......

Ni kukata miti ili kupanda mimea.

Anaonyesha kuwa wakikata miti basi bila shaka kwa ajili ya uwezo wa fedha alio nao Wangari Maathai raia watapelekwa korokoroni. Maathai ni mbunge wa eneo Bunge la Tetu aliyeshinda tuzo la Nobel mwaka wa 2004 kutokana na kampeni yake ya upanzi wa miti nchini Kenya. Kuna dhuluma dhidi ya wanyonge ambapo maskwota walioishi kwa misitu hii kwa muda mrefu walifukuzwa ili miti ipandwe.

Baada ya matamshi haya tuliona kuwa wananchi waliokuwa wakilima misituni waliandamana kwa vile walihofia kufukuzwa kwenye mashamba waliokuwa wakipanda mimea. Kwa ajili ya uwezo wa lugha matamshi ya Mheshimiwa Koigi,

mbunge wa Subukia yaliwachochea wakaazi wa sehemu hizi na yaliweza kuzua vita.

### 3.3 "Mbwa wa kisiasa"

Matamshi ya Mungatana ambaye ni mbunge wa Garsen yalielezwa na Raila kuwa kelele tu ambazo si tisho kwa Agwambo (jina la utani la Raila) likiwa na maana jogoo asiyetishwa na kuku wengine. Kile anachodhihirisha ni kuwa kuna wanasiasa wanaojulikana kwa propaganda ambao humsifu kiongozi hata ikiwa kiongozi huyo anafanya mabaya. Obeng (2002) anaeleza kuwa kiongozi wa Ujerumani Adolf Hitler alimteua Joseph Goebells kuongoza wizara ya propaganda. Kazi yake ilikuwa kufikia umma na kueleza kwa kupongeza matukio aliyoyafanya Hilter hata ingawanje yalikuwa mabovu. Hivyo basi Goebells anaweza kufananishwa na Mungatana nchini Kenya.

### 3.4 Kejeli

Mungatana anakikejeli chama cha LDP kuwa afadhali KANU iliyokuwa na sera ya kutosomesha watoto wa shule za msingi bure, lakini LDP haina sera yoyote. Inaeleweka kuwa chama cha NARC kilianzisha masomo ya bure kwa shule za msingi nchini Kenya. Anasema kuwa sera ya LDP ni kufuata mtu mmoja – mweusi ambaye ni Raila. Kwa hivyo kule kumuita Raila mtu mweusi pia ni kejeli. Kule kumuita Raila mtu mweusi inaonyesha kuwa Raila anatoka kwa jamii ya Waluo ambao ni wa Nilotiki, ilhali Mungatana ni Mpokomo ambao ni wa Bantu. Kwa hivyo

kutokana na itikadi za kijamii Mungatana alikuwa akimdharau mwenzake kwa kuwa anatoka kwa jamii ambayo inajulikana kwa kutotahiri wanaume wao.

Itikadi za kijamii pia zinaendelezwa na matamshi ya Mungatana anaposema.

> *If Raila eats fish from Lake Victoria, I eat Crocodiles from Tana River.*
>
> Raila anakula samaki wa ziwa Victoria mimi ninakula mamba wa mto Tana. (Tafsiri yetu)

Kile Mungatana anajaribu kusisitiza ni kuwa hangependa Raila kumdhalilisha kwa vile yeye (Mungatana) anatoka katika jamii inayoogopewa kwa vile wanaishi na mamba na wao huwaua mamba hao. Mungatana anajitwika sifa na hivyo anataka Raila amuheshimu.

Wakati mgombeaji wa kiti cha Kisauni kwa tikiti ya LDP aliposhindwa na Anania Mwaboza katika uchaguzi mdogo wa Kisauni na Mungatana ndiye aliye kuwa kiongozi wa kampeni ya Mwaboza: Mungatana anajisifu kwa kusema;

The crocodile has eaten the fish (Mamba amemla samaki) kwa hivyo Mungatana anajifananisha na mamba na Raila anafananishwa na samaki).

### 3.5 Sitiari

Sitiari huhusisha uainishaji wa kisemantiki ambapo dhana moja inahusishwa na nyingine ambapo lugha ya ujanja hutumika. Wakati wanapotumia sitiari wanasiasa hulinganisha dhana fulani na nyingine. Kwa mfano mtu au taifa hulinganishwa na

kifaa, mtu mwingine, mnyama ili kubainisha sifa ambazo mwanasiasa anataka kubainisha.

Ngoyani ( 2002:31) anaeleza kuwa kwa hila za Nyerere kutaka Watanzania wakatae ubepari na wakubali ujamaa, Nyerere alifananisha mali ya kibepari kama damu na kampuni za kigeni kama wafyonza damu. Aliona ubepari kama unyama na mabepari kama wanyama.

Nyerere ananukuliwa:

> Although when we talk of exploitation we usually think of the capitalists. We should not forget that there are many fish in the sea.They eat each other. The large ones eat the small ones and the small ones eat those who are even smaller.
>
> Wakati tunapozungumzia kuhusu unyonyaji huwa tunafikiria kuhusu mabepari, tusisahau kuwa kuna samaki wengi baharini, wakubwa kwa wadogo, wanakulana wenyewe kwa wenyewe.Wakubwa wanakula wadogo na wadogo nao wanakula wadogo zaidi.(Tafsiri yetu)

Obeng (2002) anaangazia sitiari ya siasa kuwa husaidia kulainisha au kuondoa kabisa hatari na vitisho vya uso katika matamshi.

Steinhart na Kitany (1998) wanaeleza kuwa sitiari husaidia kuelezea hisia na hutega usikivu wa umma. Sitiari huweza kuonyesha ukweli wa hali kwa mfano ukatili, kupendezwa, uovu, uzembe, udanganyifu, mamlaka, hekima, upuuzaji na uhaini. Sitiari huoanisha dhana zinazozungumziwa na msikilizaji na hivyo hadhira kufananisha dhana hizo.

Kwa kutumia Lakoff na Johnson (1992) mtindo wa njia mtazamo mbiii ambapo sitiari husaidia kuendeleza msamiati wa lugha ya Kiswahili na matini ya siasa. Kwa hivyo kuimarika kwa Kiswahili kunaendelezwa na sitiari. Maneno ambayo hutumiwa huwa na maana isiyo ile inayojulikana. Sitiari haiangazii tu njia ya kuangalia ukweli kwani pia huwasisimua wasikilizaji kufikiria jinsi mzungumzaji anavyotaka. Huweza kufanya hadhira kuwa na mtazamo mwingine kuhusu vitu, watu, matukio ambayo huongoza kuwa na mwelekeo mpya. Matokeo yake ni kuwa sitiari huelekeza njia ambapo mawazo na maoni ya watu hubadilika.

## 3.6 Vijembe

Katika matini ya siasa wanasiasa huongea kuhusu wenzao kwa kutumia vijembe. Mwanasiasa huonyesha tabia za mwanasiasa mwingine kwa kumfananisha na dhana nyingine. Anaweza kumkejeli mwanasiasa mwingine aidha kwa wimbo, mafumbo, hadithi ambapo huhusisha yule anayelengwa. Hadhira huwa imeelewa yule anayelengwa.

Mungatana anampiga kijembe Balala anaposema kuwa mikono nyororo ya Balala haiwezi kushika mamba, kwa hivyo Mungatana anajifananisha na mamba; mnyama mkubwa wa mto anayeogopewa.

## 3.7 Mwingiliano wa matini katika siasa

Mwingiliano wa matini ni mojawapo ya mbinu ya mawasiliano ya kisiasa. Bakhtin (1981) Inahusisha kuazima kutoka kwa matini ya awali ama inayofuata na hivyo

kubuni mpya. Matini za siasa huhusu mwingiliano wa mazugumzo na hufanya kazi kupitia kwa maagizo na kuathiriana. Inahusu mshikamano katika matini na vile vile maongezi yanayoingiliana kati ya matini na elimu ya umma husika ni dhana muhimu ya mwingiliano wa matini.

Matukio ya kihistoria kwa jamii ya mwanasiasa, itikadi ya mwanasiasa, sera zao pia maisha yao ya kihistoria (awali) yote hiyo huathiri matini ya siasa. Ili kuelewa vile hotuba huwa na mshikamano na jinsi sentensi huhusiana na nyingine vigezo vya isimu kuhusu mwingiliano wa matini Halliday na Hassan aliainisha njia tano za mshikamano;

1. Urejeshaji
2. Ubadilishaji
3. Udondoshaji
4. Mshikamano Wa Kileksia
5. Uunganishaji

### 3.7.1 Urejeshaji

Huu ni mshikamano wa kisarufi na unatokea pale ambapo kufasiriwa kwa kipengele kimoja kunategemea kipengele kingine katika matini. Yaani kuwepo na kirejeshi na kirejelewa.

### 3.7.2 Ubadilishaji

Ni mshikamano wa aina ya udondoshi na hutokea kipashio kimoja kinapobadilishwa na kingine katika matini. Kipashio kinachotumika badala ya kile cha awali kina uamilifu sawa na kile cha awali.

### 3.7.3 Udondoshaji

Ni aina ya mshikamano ambao huruhusu kuondolewa kwa neno au maneno fulani katika matini mradi tu maana yake idhihirike kutokana na matumizi ya neno au maneno hayo katika sehemu nyingine ya matini.

### 3.7.4 Mshikamano wa kileksia

Mshikamano wa kileksia hujumuisha matumizi ya uradidi, visawe na maelezo.

Uradidi huchangia katika mshikamano kwa kurudia kipashio fulani katika matini.

Rais Kibaki ana wanawake wawili, NAK na LDP. NAK ndiye anayependwa sana.

Chama cha NAK kimerudiwa katika sentensi hizi.

Beugrade na Dressler (1981) wameongeza aina nyingine za uradidi. Uradidi usio wa moja kwa moja na uradidi sambamba. Katika uradidi usio wa moja kwa moja neno fulani hurudiwa katika matini lakini likiwa katika kategoria tofauti na lile la awali kwa mfano;

Raila na Mungatana walisafiri kwa ndege kwenda Mombasa. Safari yao ilichukua saa moja. Walisafiri ni kitenzi lakini safari ni nomino. Uradidi sambamba nao

unahusu urudiaji wa utaratibu fulani lakini kwa kutumia vipashio tofauti. Rais aliwapa mawaziri mamlaka ya kuteua, kufuta na kuadhibu mfanyi kazi yeyote.

### 3.7.5 Uunganishaji

Katika mshikamano huu, vipashio vya lugha hutumiwa kuleta uhusiano ama ndani ya sentensi au baina ya sentensi uunganishaji unachangia mshikamano kwa kutumia vile viunganishi vya aina mbalimbali kama vile na, lakini, ingawa, tena, kwa sababu na kwa kuwa. Wakati wa uchaguzi wa kisauni baada ya kifo cha mjumbe Maitha, Mungatana alisema.

> We settled for Mr. Anania Mwaboza because we understood what kind of person he is and how best he could push the coast agenda especialy the land issue.
>
> Tuliamua kumuunga mkono Bwana Anania Mwabonza Kwa vile tulijua ni mtu wa aina gani na jinsi angeweza kusukuma ajenda ya watu pwani hasa kuhusu mashamba. (Tafsiri yetu)

Maneno **kwa vile** na **na**, yametumiwa ili kuunganisha sentensi katika matini hiyo. Pia inadhihirika wazi kuwa kuna shida ya mashamba mkoa wa pwani ambapo ni maudhui yanayojitokeza. Watu wa Pwani walinyang'anywa mashamba na watu kutoka nje. Uunganishaji kuhusu jinsi sentensi zinavyoingiliana na hujiendeleza kwa ajili ya kuwania kisemantiki. Uunganishaji unaweza kuwa wa kuongezea au kuendeleza usemi usio rasmi.

Bwana Mungatana alikuwa akimpigia debe Bwana Anania Mwaboza aliyekuwa akiwania kiti cha ubunge cha Kisauni. Swala nyeti zaidi katika eneo la Pwani ni

swala la mashamba. Lugha aliyoitumia Bwana Mungatana ilimsawiri Mwaboza kama mkombozi wa watu wa eneo hilo kwa kuahidi kushughulikia maswala ya mashamba. Watu wa eneo hilo walivutiwa sana na ahadi hiyo na kuweza kumuunga mkono kwa wingi Mwaboza.

Mazungumzo yanaweza kuanishwa ifuatavyo Kwa mfano matini ya Kamotho; Kamotho ndiye Mwandishi Mtendaji wa chama cha LDP na ni mbunge wa Mathioya. Kwa ajili ya cheo chake chamani anapozungumza basi bila shaka ni msimamo wa chama hicho.

> Our support to the people driven constitution review process and we support the work done by the Kenyan people at Bomas. The Bomas draft is the people's draft. We therefore call upon the Attorney General to move speedily to enact the constitution and publish the draft constitution without further delay and table it in Parliament quickly. L.D.P reinstates that NARC is a coalition of parties. LDP recognizes only corporate membership of NARC and rejects any attempts of NARC as a monolithic party and with individual membership purpoted recruitment is illegal and will be resisted by Kenyans.
>
> LDP upholds the directive by Hon. Murungi on party elections and filling of returns. LDP will be guided by partys constitution and instructions from registrar of societies but not by threats from party activists. LDP belief that directives of the minister and are divertionally intended to remove the spotlight from the corruption by high level government officials and ministers.
>
> Recruitment of members to political parties LDP will continue with mass recruitment of members until the end of April 2005 when the Party will announce a time table for grassroot and national election.

The threats of Hon Kiraitu not withstanding but I must also add here that returns of LDP are upto date. We have nothing to make returns on. LDP calls upon the office of the president to speed up the issuance of National Identity cards irrespective of their regions to qualified Kenyans. The current registration of persons programme is assuming emergency status in certain regions when it has virtually stalled in other regions which are perceived not to be politically correct. We call upon the registrar of persons to act independently of presidents office to avoid political interference in the registration of persons and they should also register in areas perceived as opposition region.

Tunaunga mkono mabadiliko ya katiba yanayoendelezwa na wananchi na pia kazi iliyofanywa na Wakenya kule Bomas. Mswada wa Bomas ni wa watu wa Kenya kwa hivyo tunamshinikiza Mkuu wa Sheria bila kuchelewa kuuwasilisha bungeni.
LDP inashinikiza kuwa NARC ni muungano wa vyama na pia inakubali kuwa uwanachama wa NARC ni wa kishirika na sio wa kibinafsi kwa hivyo hatua ya usajili wa wanachama wa NARC ni wa haramu na utakataliwa na Wakenya.

LDP inapinga maagizo ya Mheshimiwa Kiraitu Murungi kuhusu uchaguzi wa vyama na mawasilisho ya hesabu kwa hivyo LDP itaelekezwa na katiba ya chama na maagizo kutoka kwa msajili wa vyama lakini sio vitisho kutoka kwa wahamasishaji watendaji wa vyama. LDP inaamini ya kwamba maagizo ya waziri yananuia kuchepua kuangazia maswala ya ufisadi wa hali ya juu wa maafisa wa kiserikali na mawaziri.

LDP inanuia kuendeleza kuandikisha wanachama hadi mwisho wa Aprili 2005 wakati ambao chama kitatangaza ratiba ya uchaguzi wa mashinani na wa kitaifa. Hatujali vitisho vya Mheshimiwa Kiraitu kwa vile hesabu zetu kama chama ziko sawa.

LDP inahimiza afisi ya rais kuharakisha utoaji wa vitambulisho vya kitaifa kwa wananchi bila kujali sehemu wanazotoka. Usajili wa watu hivi sasa unafanywa kimapendeleo kwa kutoa vitambulisho kwa

watu wa sehemu zingine na kuwacha zingine zinazochukuliwa kuwa za upinzani. Kwa hivyo tunamhimiza Msajili wa Watu afanye kazi bila kutegemea maagizo kutoka kwa afisi ya rais na atoe vitambulisho kwa maeneo yanayochuliwa kama ya upinzani. (Tafsiri yetu)

## 3.8 Maelezo.

Msamiati uliotumiwa ni wa kushawishi Kwa mfano maneno kama:

(*We call upon.....)*

Sentensi zilizotumiwa ni ndefu ndefu

Viunganishi vimetumiwa; neno lililotumiwa ni; and, but

### 3.8.1 Eksofora.

Urejeshi wa eksofora hurejelea vitu vilivyo nje ya matini. Hivi ni vitu vilivyo kwenye mazingira au visivyo dhahiri kwenye matini. Urejeshi huu kwa mujibu wa Brown na Yule hautaji vitu kwa majina mara nyingi lakini huashiria tu.

K.M ........without further delay tables *it*

'It' inaashiria katiba.

### 3.8.2 Visawe

Visawe pia vimetumiwa. Visawe ni neno au kishazi chenye maana sawa na neno au kishazi cha awali. Kwa mfano *not politically correct* ni kisawe cha *opposition region.*

### 3.8.3 Maudhui

Kutokana na matini tunaweza kufasiri maudhui ya ujumbe ambapo kuna migogoro kati ya matapo mawili ya vyama vya siasa. Mizozo kuhusu katiba, uchaguzi wa vyama, uandikishaji wa wanachama na pia kuhusu kutolewa kwa vitambulisho kwa baadhi ya sehemu na kutoshughulikia sehemu zingine.

Hatua hii ya maelezo inahusu kutoa maelezo au kuelezea sifa za matini. Hapa ni kutazama msamiati na kuona msamiati uliochaguliwa, istiara zilizotumiwa, visawe, tasfida, kejeli na vijembe. Pia kuangalia sarufi na kuchunguza aina ya sentensi zilizotumiwa kwa mfano sentenzi fupi au changamano. Unominishaji uliyotumiwa katika matini na umatini kama vile anaphora na deksisi.

### 3.8.4 Ufafanuzi

Utanzu uliotumiwa ni taarifa kutoka chama kilicho serikalini cha LDP ambacho kimeghadhabishwa kuhusu kutoasilishwa kwa katiba. Wakati wa kampeni wanasiasa walitoa ahadi kuwa wangewapatia Wakenya katiba mpya siku mia moja baada ya kuchukua uongozi wa nchi. Lakini ilikuwa zaidi ya mwaka lakini ahadi hiyo ilikuwa haijatimika.

Mzungumzaji ni katibu mkuu wa chama cha LDP ambacho kilikuwa serikalini kwa hivyo ilidhihirika wazi kuwa kulikuwa na mzozo serikalini. Pia msemaji ni mwanamme katika jamii ya Kiafrika. Hivyo basi kuhusu nguvu alikuwa katika

tabaka aali. Uwezo huu ulimwezesha kufikia uneni kwa mfano kutumia vyombo vya habari ili kueneza msimamo wa chama kuhusu katiba, uchaguzi wa vyama, uwasilishaji wa makadirio ya fedha ya vyama na kuhusu uandikishaji wa wanachama wa vyama.

### 3.8.5 Ufafanuzi Elezi

Huu ndio ulikuwa msimamo huhusisha masharti ya jamii kama vile masharti ya jamii ya uzalishaji na masharti ya jamii ya uchambuzi au ufasiri. Masharti hayo yanahusiana katika viwango tofauti vya jamii. Masharti haya matatu ya jamii huchonya au hujenga jinsi watu huzalisha na kufasiri na ndiyo inayoeleza jinsi mazungumzo huzalishwa na kufasiriwa.

### 3.8.6 Hitimisho

Kulingana na utamaduni wa jamii husika sitiari, vijembe, kejeli hueleweka kuwa ni matamshi ya maana ingawaje hukiuka kanuni za kisemantiki na pragmatiki. Hata hivyo sitiari huwasilisha dhana zilizo na maana ambapo inaweza kufasiriwa kwa njia tofauti. Wanasiasa huwasilisha dhana kwa njia isiyo dhahiri au wazi ili kuhifadhi na kuendeleza amali zao ili kupata mamlaka ya kisiasa, kiuchumi na kujinufaisha dhidi ya wapinzani. Wanasiasa hutumia njia hizo hizo ili kuhifadhi mamlaka.

# *SURA YA NNE*

## 4.0 DHIMA YA LUGHA KATIKA MATINI YA SIASA NCHINI KENYA

### 4.1 Utangulizi

Kuanzia mwaka wa 2002, kumekuwa na matumizi mbalimbali ya lugha katika siasa yanayoelekezwa kupata manufaa fulani kisiasa. Lugha hiyo imekuwa ikibadilika siku baada ya siku kadri mandhari ya kisiasa yanavyobadilika. Mwaka wa 2002, ulishuhudia matumizi ya lugha yalijikita hasa katika kuchochea wananchi dhidi ya chama cha KANU na kushawishi wapiga kura.

Mwaka uliofuatia, lugha hiyo ilibadilika na ikawa ya kushurutisha na kuomba kupewa muda kwa serikali mpya ya NARC. Mwaka 2004 na kuendelea, maswala muhimu ya kikatiba yaliibuka na yakazua hisia mpya miongoni mwa wanasiasa, serikali na wananchi.

Kinachoibuka ni kuwa lugha hubadilika kufuatia matukio mbalimbali. Lugha ya wanasiasa imechukua sura nyingine ikawa ya kusuta, kukejeli, kukashifu, kujitapa, kuonya, kueleza na kukosoa. Picha inayoibuka ni ya wanasiasa walioridhika na mamlaka waliyoyapata kwa njia ya kisiasa, na wale ambao hawakuridhishwa na mamlaka yaliyoko hususan wale ambao hawakupata vyeo katika serikali mpya na wale ambao maeneo yao hayakufaidika kutokana na serikali hiyo.

Wanasiasa wa kipindi hiki (2002-2005) walitumia lugha kutimiza mambo mbalimbali. Jambo la kwanza na la umuhimu mkubwa lilikuwa ni kung'oa chama

kilichokuwa kikitawala cha KANU mamlakani. Lugha yenye mnato, kusihi kukashifu na kuahidi.

## 4.2 Ahadi

Ahadi zilizotolewa na chama cha NARC zilikuwa nyingi na za kuvutia wapiga kura. Chama hicho kilikuwa na wasemaji waliobobea katika matumizi ya lugha, akiwemo hayati makamu wa Rais Kijana Wamalwa aliyetumia lugha yenye mnato zaidi na kuvutia hisia za wananchi. Mfano mzuri ni hotuba aliyotoa katika mkutano wa viongozi wa vyama vya upinzani kabla ya uchaguzi mkuu, Mkutano uliofanyika katika hoteli ya Hilton, mjini Nairobi.

> Leo, tunaiandika historia ya Kenya upya kwa herufi za dhahabu. Kufahamu kwetu wale walioko katika upinzani kwamba ili kuiweka nchi yetu huru kutoka kwa umaskini usio kifani na maanguko makuu ya kiuchumi, kijamii, kisheria na njia nyinginezo zote, lazima tuungane kama watu werevu na tufanye kazi pamoja, tupigane pamoja ili kutoa serikali hii ya (KANU) mamlakani. Nina ukweli katika kitabu ninachoandika kuwa enzi ya nyayo ilikuwa makosa makuu. Mabibi na mabwana, sisi katika upinzani lazima tuwafanyie vyovyote watoto wa Kenya bali sio kwetu mtakuwa dhahiri tu, iwapo tutakubali msimamo mmoja. Kwamba watoto wetu hawajamkosea yeyote, ilhali tunawaharibia maisha yao ya baadaye. Iwapo yeyote atazidi kuwanyanyasa hata nikiwa mimi basi njia ya kunimaliza inapaswa kutafutwa. Tutaweza tu kufaulu iwapo sisi viongozi tutaweza kutupilia mbali ubinafsi na kusema kuwa tutafanya kila kitu kwa sababu ya watoto wa Kenya....

Hotuba hiyo ya Bwana Wamalwa ilipelekea wanasiasa wa vyama vyote vya upinzani kuungana na kutoa kiongozi mmoja aliyeng'ang'ania kiti cha urais dhidi ya

mwakilishi wa chama cha KANU, Bwana Uhuru Kenyatta. Hotuba hiyo, ambayo iliingia katika historia kuwa moja ya bora zaidi kuwahi kutolewa, iliwanyamazisha wananchi wa maeneo mbalimbali waliokuwa wakiwapigia viongozi wao debe kugombea kiti cha Urais kwa tiketi za vyama vyao.

Siasa ya mwaka wa 2002 ilioona matumizi ya lugha iliyoibua hisia mpya ya matumaini kwa Wakenya wengi, hasa wale wa tabaka la chini na mapato duni. Lugha iliyotumiwa ililenga kuwapa matumaini makubwa watu ili wapigie chama fulani kura kwa wingi. Chama cha NARC kiliwaahidi Wakenya kuwa kitabuni nafasi elfu mia tano za kazi kila mwaka. Jambo hili liliwapelekea Wakenya wengi ambao hawakuwa na kazi kukipigia kura chama hicho. Lugha yenye kuibua hisia za matumaini hasa ilitumiwa kuwaahidi Wakenya mambo mengi yakiwemo nyongeza za mishahara, uimarishaji wa usalama, kilimo, biashara na hali ya maisha kwa jumla. Lugha hiyo hubuni miundo tambuzi katika akili za watu na kuwapa matumaini makubwa, jambo lilowapelekea kutenda mambo kwa kiwango fulani cha maisha.

Ahadi hizo pia zilielezwa kuwa za uongo na Mheshimiwa Uhuru Kenyatta katika mkutano wa kampeni uliokuwa uwanja wa Tononoka mjini Mombasa, na alisema hivi;

> Hakuna shortcut, hakuna shortcut ambayo itakuweko. Wengine wanaweza kuja kuahidi kuwa kutakuwa free hii, kwa mfano elimu ya bure, maji ya bure, sitima ya

> bure; ndugu zangu hakuna kitu cha bure nchini Kenya.

Ahadi hizo zilidhihirika kuwa za uongo kwa sababu NARC ilipochukuwa uongozi ahadi hizi hazikutekelezwa; kama vile Mbunge wa Kisumu Mashambani Ken Nyagudi aliposema;

Tukienda shuleni tuliambiwa ukipata 0 kwa 10 tuliambiwa umepata mtungi.

> Mou=sufuri
> Kazi 500,000=sufuri
> Majumba 150,000 kwa mwaka=sufuri
> Ole wangu, muungano wa NARC umepata sufuri kwa ahadi zake.

## 4.3 Matumaini

Umaskini katika nchi ya Kenya ulikuwa umekithiri na kufikia kiwango kikubwa sana. Lugha iliyotumiwa na wanasiasa mnamo mwaka wa 2002 ilinuiwa kugusia shida za wananchi. Waliotumia lugha hiyo walikuwa wanajua matokeo ya matumizi ya lugha kama ile. Jambo hili lilizungumziwa na Edelman (1977:154).

> Na suluhisho la umaskini huwa inaweza kubashiriwa kama umaskini wenyewe. Katika siasa, kama vile katika dini, lisilo Umaskini ni donda ndungu linaliathiri jamii zote na lugha ya kisiasa inayozungumzia kiini, madhara, wahasiriwa wa kawaida hutilia nguvu imani bila kujali uhalali wa imani hiyo.(Tafsiri yetu)

Kwa kutumia lugha inayolenga kutoa suluhisho la umaskini, wanasiasa walijua kuwa watapata wafuasi wengi, kwa sababu watu hufurahia kusikiliza na kufuata jambo lolote ambalo linazungumzia suluhisho la umaskini wao.

## 4.4 Uchochezi

Lugha iliyotumiwa hasa na vyama vya upinzani ilikuwa ni lugha ya kuchochea wananchi dhidi ya chama cha KANU na viongozi wake, ilikuwa lugha ya kupinga yote yaliyofanywa na chama hicho na utawala wake. Charity Ngilu, mwanasiasa wa NARC alisema haya kuhusu serikali ya KANU.

> Leo ni siku ya furaha kwa kila mmoja wetu. Kwa miaka kumi tumekuwa tukitafuta njia ya kujiondoa katika minyororo... vile Moi ametuweka tuwe watumwa. Lakini yeye Moi aliona kuwa anaweza kutuletea mtu aendelee kuongoza nchi ya Kenya vile yeye alivyokuwa akiongoza.

Katika mkutano wa kisiasa uliofanyika mjini Kisumu, Bwana Joab Omino aliendeleza uchochezi kwa maneno yafuatayo.

> Ikiwa tuna serikali ambayo ina uhuru Kenyatta kama President, ina Jirongo kama vice-president na Ruto kama Prime Minister na Sunkuli ndio Chief Advisor, hiyo ni serikali gani? Tunataka tuwaponde, tuwasiage kama unga, halafu tuwapeleke yamo.

Naye David Mwenje, aliyekuwa akiwania kiti cha ubunge cha Embakasi, katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika uwanja wa Kitaifa wa Nyayo, alisema yafuatayo kuhusu uchaguzi mkuu na tetesi kuwa Bwana Moi angekatalia mamlakani;

> Haya, haya, leo ni leo, msema kesho- ni muongo leo nimefurahi kwa sababu nilikuwa nafikiri hapa mahali nimesimama ni Moi tu anaruhusiwa kusimama. Na leo kumbe yote yawezekana bila Moi. Wewe chukua televisheni ili Moi aone kuwa nimesimama. Mimi maoni yangu ni hii, kwamba tumeshinda uchaguzi ambao unakuja. Nasikia rumours eti Moi anaweza

> sema anaweza katalia ofisini. Watu wa Nairobi tunasema hivi, wakati uchaguzi utatangazwa tumeshinda, tutaenda state house na kumtoa kwa nguvu...

Hotuba ya Bwana Mwenje ilionyesha mafanikio yaliyokuwa yamepatikana kwa sababu ya kishindo cha muungano wa vyama vya kisiasa huku akitabiri ushindi wa chama cha Narc na kutoa wito kwa wananchi wawe macho dhidi ya mbinu zisizokuwa za haki ambazo zingetumiwa na Rais Moi kukatalia mamlakani. Kuwaonyesha watu uwezo alio nao wa kutwaa mamlaka wakitumia njia zozote zile iwapo ya kidemokrasia ingegonga mwamba.

Uchochezi pia unadhihirika baada ya uchaguzi ambapo kulikuwa na mvutano kati ya Mheshimiwa Najib Balala mbunge wa Mvita na meya wa Mombasa, Taib. Balala alitamka yafuatayo katika uwanja wa Tononoka,tarehe 11/3/2004;

> Nawambia Balala hatingishwi. Nimechaguliwa na watu wa Mvita na kuchaguliwa kama waziri wa nchi ya Kenya, kwa hivyo mtu yeyote athubutu kuja kwa eneo bunge langu kuandikisha wanachama, tutawachoma.

Balala alitumia lugha ya uchochezi ili kuonya wanasiasa wa tapo la NAK waliokuwa wakifanya usajili wa wanachama wao.

### 4.5 Kutahadharisha

Chama cha KANU hakikuachwa nyuma katika kutafuta nafasi nyingine ya kuongoza nchi. Wanachama wake pia walikuwa na lugha yao iliyokusudiwa kuleta mafanikio

katika uchaguzi mkuu wa 2002. Bila shaka chama hicho kilikuwa kimefumaniwa na kishindo cha muungano wa vyama vya upinzani. Lugha walioitumia ilikuwa ni lugha ya kupambana na hali ya wasiwasi na hatari kubwa iliyokuwepo ya kupoteza uongozi. ikabidi viongozi wa chama hicho kutumia lugha ya kuonya watu na kuwatahadharisha juu ya yale yangewakumba iwapo wangekichagua chama cha NARC. Rais mstaafu Daniel Arap Moi alikuwa na haya ya kuwambia wananchi;

> Hata mimi nitafanya kampeni kwa chama cha KANU. I mean well all for Kenyans. I am a nationalist, not a tribalist. Msiwakubali kwani kijana anakwambia I love you, I love you, lakini yote ni uongo. Niliwaambia hadithi moja ambapo kijana anamwambia msichana kuwa I love you. I can jump over fire (kicheko).... Na akaandika kuwa I will see you on Saturday if it does not rain. Mapenzi gani hiyo kwani hawezi kuja kwa mvua? Ni ya bure.

Daniel Moi alinuia kuharibu kile ambacho muungano wa upinzani ulikuwa umejenga kwa wananchi, kwa kuonyesha kuwa watu wasiomaanisha kile ambacho wanakisema na pia wasioweza kutimiza ahadi waliokuwa wametoa. Lugha aliyoitumia ilinuiwa kuhifadhi mamlaka ya chama cha KANU na lugha maalum inayotumiwa na viongozi kuwachora wapinzani kama wakengeushi waliopotoka na kukosa mwelekeo.

### 4.6 Kuzindua

Kadiri wakati ulivyosonga, lugha ya siasa ilizidi kukua na kuchukua sura mpya siku baada ya siku. Wanasiasa wakawa wanatumia lugha ya kuwanasua watu

kimawazo ili kuamini kuwa vyama vyao vilikuwa na haki ya kuongoza. Baadhi ya viongozi walitumia lugha iliyokithiri matumaini kwa wapiga kura. Raila Odinga alitabiri ushidi wa NARC, bila shaka akikusudia kutia KANU kiwewe na kuinua nafasi ya NARC ili kuchukua uongozi:

> Narc itakuwa jahazi yetu ya kuvuka Canaan. Ulafi wa siasa haiwezi kupeleka mtu mahali. Wakati unafika kuwa usome maneno ya ukuta na uelewe na usome maneno ambayo yako ukutani.

Bwana Raila alikuwa akitabiri hatima ya chama cha KANU, na kuwahimiza watu kujiunga na chama cha NARC ambacho kingewaletea mafanikio mengi. Ni dhahiri kuwa matumizi ya lugha yanuiwa kutimiza malengo mawili makuu, kutafuta wafuasi na kuendeleza upinzani.

Bila shaka matumizi mengine ya lugha yalionyesha ubunifu mkubwa wa kisiasa. Mwai Kibaki aliibuka na ahadi zilizoridhisha nyoyo za wapiga kura wengi. Ahadi hizo ziligusia maswala ya umuhimu mkubwa katika maisha ya kila siku ya mwananchi.

> Serikali yangu itatoa elimu ya bure katika shule za msingi. Kuhusu ukosefu wa kazi, lengo letu ni kufufua viwanda na kusaidia wakulima. Pesa zinazolipwa kama kodi zisiporwe. Ufisadi tutapigana nao. Ili kupigana na ufisadi, lazima wale waliopewa madaraka lazima watangaze utajiri wao.

Bwana Mwai Kibaki aligusia kile ambacho watu walikuwa wakitaka kusikia, mabadiliko katika sekta zote za maisha yao, huku wakiahidiwa na kutarajia mwamko mpya katika maisha. Lugha aliyoitumia ilisheheni matarajio makubwa hasa ikitiliwa maanani kusambaratika kwa asasi zote ambazo zingeweza kumnufaisha mtu wa kawaida. Bwana Kibaki alizungumzia maswala nyeti yaliyogusia maisha ya watu, na akatumia lugha waliyokuwa wakitaka kusikia wakati huo, ambayo ni huduma za bure. Ahadi alizotoa ziliinua matumaini ya Wakenya wengi, hasa wale wenye mapato ya kiwango cha chini na wasiokuwa na kazi na yakawapa watu hao motisha wa kumpigia kura za urais. Bwana Kibaki alichora picha ya serikali yenye utendawazi na ya kutenda kazi. Aliungwa mkono sio tu na raia wa kawaida , bali pia viongozi wengine wakisiasa.

## 4.7 Changamoto

Lugha ya kuwapa changamoto wananchi ilitumiwa katika kipindi hicho. Nia hasa ilikuwa ni kuzindua upya fikra za watu ili waanze kuona mwamko mpya.

Michael Kijana Wamalwa hakusita kutumia mbinu zote za lugha kuhakikisha kuwa chama chake cha Narc kilipata wafuasi, katika mkutano uliofanyika katika uwanja wa kitaifa ya Nyayo,

> Hakuna Mkenya ambaye hangependa kuiacha Kenya au kubadilishana uraia na watu wengine kwa sababu we are on the threshhold of one of the major human revolution. Kutoka serikali mbaya ambayo imeendesha nchi yetu kwa kupiga hatua ikirudi nyuma mpaka tukafikia kiwango cha stone age, na sasa tutaipiga teke tuandike serikali ambayo itatuendeleza mpaka we reach the sky....

Bwana Kijana Wamalwa alizungumzia mambo yaliyokuwa yakijiri kana kwamba hatima ya Wakenya ilitegemea hotuba hiyo. Aliweza kusawiri, kwa kutumia lugha, hali ya kutamauka iliyokuwa imekita mizizi nchini Kenya, kufikia kiwango cha Wakenya wenyewe kutoona ugumu wowote kuihama nchi yao. Hotuba hiyo iliyozua hisia kali ilikuwa ombi kwa Wakenya kuchukua mwelekeo mpya wa kisiasa na kuwapa matarajio makubwa iwapo wangetekeleza ombi hilo. Alifanikiwa sana katika ombi lake kwani kwa mara ya kwanza wananchi pamoja na viongozi walitupilia mbali uhasama na ubinafsi kwa minajili ya kuungana na kukiangusha chama cha KANU.

Wakati huo pia ulishuhudia matumizi ya lugha kiweledi na baadhi ya wanasiasa waliokomaa katika matumizi ya lugha. Bila shaka yao ilikuwa ni njia iliyoamuliwa kabla, ya kuhakikisha matokeo fulani katika uchaguzi mkuu na kuwaathiri Wakenya kwa njia ya kudumu. Wanasiasa hao ambao wana kiwango cha juu cha elimu walitumia uwezo wao wa kielimu na kubuni lugha iliyowaathiri kwa kiwango kikubwa watu ambao wameelimika. Daktari Mukhisa Kituyi na Michael Kijana Wamalwa walijitokeza zaidi katika mtazamo huu. Wamalwa alitumia maneno yafuatayo katika mkutano uliofanyika katika uwanja wa kitaifa wa Nyayo.

> Mimi ni mtu mkarimu sana kwa kawaida, lakini nimejaribu kufikiria jambo moja zuri ninaloweza kulisema kuhusu utawala wa Moi na sijalipata. Ningekuwa Rais Moi, wakati . huu anapokodolewa macho na hali ya kusahaulika kabisa kwa sababu ya kutokuwa na mafanikio yoyote, singesubiri hadi Januari 5. Ningetoka katika ikulu huku nikiwa nimeficha kichwa changu kwenye suruali. Wananchi

> watukufu, wenyewe mtajionea serikali tofauti, na mimi namuombea Rais Moi maisha marefu aende Baringo akafukuzane na mbuzi zake na aone vile serikali ya kuwahudumia wananchi inavyoendesha kazi.... Wananchi watukufu, serikali mpya ya rais Kibaki itahitaji kazi na challenge ya kila Mkenya ni kila mmoja achangie kurejesha nchi hii kuwa nchi ambayo inaheshimiwa duniani. Kila mmoja wenu atakuwa balozi wa Kibaki kuomba kura. Tungependa kusihi kila mtu tarehe ishirini na saba, mwezi wa kumi na mbili mwaka wa elfu mbili na mbili, kila mtu aliyeshika kura apige kura. Akiwa mgonjwa, bora asiwe mahututi sana, tumuweke kwa wheelbarrow na tumpeleke apige kura.

Katika hotuba hii, Bwana Wamalwa aliweza kutumia lugha yenye kuchora picha ya kuogofya kuhusu serikali ya KANU iliyokuwa ikitawala wakati huo. Alichora utawala wa Moi, kuwa usiokuwa na manufaa yoyote kwa Wakenya na huku kutabiri ubora wa serikali ya Bwana Kibaki kwa kuchora picha ya mafanikio makubwa iwapo chama cha NARC kingepata nafasi ya kuongoza nchi. Hotuba yake ilikuwa kana kwamba tayari chama chake cha NARC kilikuwa kimehakikishiwa ushindi. Aliwasihi watu kujitokeza kwa wingi kukipigia chama cha NARC kura na kwa hakika tarehe aliyoitaja yaani tarehe 27.12 2002, Wakenya walijitokeza kwa wingi na kukipigia chama cha NARC kura nyingi sana. Hivyo basi alifaulu kuwaonyesha watu umuhimu wa kukichagua chama cha NARC na manufaa ya kukataa chama cha KANU.

Mazungumzo ya Wamalwa yalizua azma mpya na kuchochea wapiga kura kutimiza yale aliyoyasema kwa minajili ya kubadilisha nchi. Baada ya uchaguzi, NARC

ilikuwa imepata ushindi mkubwa na Kibaki kuchaguliwa kuwa rais wa tatu wa Jamhuri ya Kenya.

Baada ya uchaguzi huo, lugha ya wanasiasa ilichukua mwelekeo mpya, ambao ulikuwa tofauti kabisa na ule wa kabla ya uchaguzi. Wanasiasa wakachukua mirengo tofauti katika mazungumzo yao. Lugha hiyo ilibadilika kwa sababu za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Chama cha NARC kilishinda uchaguzi mkuu wa 2002, na kupata uwezo na mamlaka ya kutawala. Jambo la muhimu zaidi kukumbuka ni kuwa ahadi zilizotolewa na chama hicho wakati wa kampeni zilipelekea wananchi kupigia chama hicho kura. Lugha iliyotumiwa ilisheheni matumaini makubwa sio tu kwa mwananchi wa kawaida, bali pia kwa wawekezaji na jamii ya kimataifa. Ahadi zilizotolewa ni kama vile kuwepo na katiba mpya ndani ya siku mia moja ya kupata mamlaka, kuongeza mishahara ya polisi, walimu, wafanyi kazi wa serikali na wale wa vyuo vikuu. Uimarishaji wa ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, kumaliza ufisadi, kupambana na uhalifu, uimarishaji na utambuzi wa haki wa kibinadamu na ukuaji wa kiuchumi kwa jumla. Baadhi ya ahadi hizo zilitimizwa kwa kiwango fulani.

## 4.8 Katiba

Swala lililozua kasheshe ni lile la katiba, kwa kiwango cha kutishia kusambaratika kwa serikali ya NARC. Lugha mpya ikaibuka kufuatia mabishano ya katiba mpya. Viongozi wa kisiasa na kundi lililopewa mamlaka ya kufanyia katiba marekebisho wakaanza mabishano makali mno. Kwa hivyo baada ya uchaguzi mkuu, lugha

iliyotumika ilikuwa ni ile ya kujitapa, kukashifu, kusuta, kukejeli, kulaumu kujisifu na kutamauka hasa miongoni mwa wale ambao hawakufanikiwa kupata mamlaka katika serikali mpya. Maneno yafuatayo yalitamkwa na Joseph Kamotho, nyumbani kwake huko Mathioya wakati wa sherehe za kusherehekea ushindi wake;

> Na wale wengine ambao hawakuwa wametosheka na uongozi wa serikali ya KANU tukazunguka Kenya nzima tukaenda Machakos, Kitui, Mombasa, Nairobi, Kapsabet, Eldoret, Thika.. Mikutano mikubwa mikubwa, na wananchi wakatuomba tuungane pamoja na tuwe na mtu mmoja tu wa kupigania kiti cha rais wa Jamhuri ya Kenya na tukasema lazima tuzungumze na watu wa NAK, na tukaenda kila mahali na muungano wa Rainbow. Mambo ya chama cha KANU wakasema iwe ni historia watoto watasoma baadaye . Kama hapa kuna mtu ambaye anaweza kutetea chama cha KANU vile mimi nilitetea aje hapa. Ni mimi tu niliweza kutetea chama hicho. Lakini ukifika mahali unanyima watu demokrasia utaachwa pekee yako... Na kwa hivyo watu wa Mathioya, Murang'a na kila mahali wale wanaendelea kushikilia chama cha KANU ni kama kupe hata ngombe anapokufa hukaa kwa ngozi.. ukumbuke nilisema nini wakati walisema mtoto wa Kenyata anaweza kutuongoza. Mtoto wa nyoka ni nyoka.

Hapana shaka kuwa Bw. Kamotho alikuwa akijisifu kutokana na ushindi huo wa chama cha NARC na kuona busara aliyokuwa nayo katika kukihama chama cha KANU.

Punde tu baada ya serikali kuundwa, mizozo ilianza ndani na nje ya serikali. Lugha ya kutoridhika ikachukua usukani. Kuna wale walioona kuwa wameachwa nje ya serikali, au hawashirikishwi kikamilifu katika maamuzi fulani ya umuhimu mkubwa.

Bw. Raila Odinga akizungumza juu ya mizozo ndani ya chama cha NARC alikuwa na haya ya kusema kuhusu makabiliano baina ya vyama tanzu vya NARC.

> Iwapo una bibi wengi, lazima uwapende wote la sivyo utaleta hali usiyoweza kuimudu. Ukionyesha mapenzi tu kwa watu fulani katika jamii, mtafaruku lazima utatokea.

Mizozo ndani ya chama cha NARC iliendelea kushamiri huku kila mwanasiasa aliyehusika akitaka atoe maoni yake na pia yatiliwe maanani. Hali hiyo ilileta taharuki baina ya washika dau wa chama hicho. Bwana Christopher Kirwa mbunge wa Cherengani, alitoa maoni yake kuhusu yale yaliyokuwa yameibuka.

> Hakuna mgawanyiko katika chama cha Narc. Hakuna vita ndani ya baraza la mawaziri. Yale tunayoyasikia ni makorofishano madogo madogo kawaida ya familia ya wake wengi. Katika serikali ya muungano lazima kuwe na minong'ono. Lazima watu wakohoe. Lakini kulia kwa chura hakuwezi kumnyima ng'ombe maji. Ng'ombe atakunywa maji na wakati mwingine abojoke hayo maji na aende zake hata kama chura amepiga makelele kwa sauti ya juu kiasi kipi.

Lugha aliyoitumia ilikuwa ni ya kuwaonya wale ambao hawakuridhishwa na kuteuliwa kwake kama waziri na pia kutupilia mbali mazungumzo ya kuanguka kwa serikali mpya. Hata hivyo, kuna wale wanasiasa ambao walihisi kuwa mambo hayakuwa yakienda itakikanavyo katika serikali. Naye Bw. Kijana Wamalwa akawa na haya ya kusema;

> Msiwe werevu miongoni mwenu, kwa kucheza karata juu ya meza huku mkiwa mmeficha kadi za hatari chini ya meza.

Mzozo mkubwa uliibuka baina ya vyama tanzu vya NARC hasa kati ya LDP, DP na NPK, kwa sababu ya kutotiliwa maanani kwa mkataba wa makubaliano jambo hilo halikuchukuliwa kwa njia nyepesi na baadhi ya viongozi. Maina Kamanda alikuwa na haya ya kusema juu ya mnong'ono na chama cha LDP;

> Shida ya LDP ni kuhusu miungu wadogo wa chama hicho.

Mizozo hiyo ilipelekea baadhi ya wananchi kukata tamaa na hawangeweza kuona tofauti ya chama cha NARC na kile cha KANU, jambo ambalo lilikanushwa vikali na Kiraitu Murungi akikitetea chama na uongozi wa NARC;

> Kulinganisha NARC na KANU ni kama kulinganisha usiku na Mchana. Hii serikali ya kufanya kazi. Serikali ya uongo, ufisadi tuliondoa. Kwa hivyo kama kuna wengine wamebaki hapa, tafadhali padre wafanyie maombi waokoke kwa sababu tunataka Kenya mpya... Tunataka watu wetu wainuke watoke kwa ufukara, matopeni waingie katika demokrasia, wawe wananchi ambao hawana shida yeyote.

Hofu kuu iliwakumba wananchi na wanasiasa baada ya kuona kuwa katiba mpya haitatolewa katika ule muda uliowekwa. Kiasi kikubwa cha pesa kilitumiwa katika mikutano ya kujadili katiba mpya. Wingu la manung'uniko lilitanda kote. Mheshimiwa Macharia Mukiri mbunge wa Ndaragua alitetea serikali vikali kuhusu swala hilo. Bila shaka lugha aliyotumia ilikuwa ya uchochezi na matusi;

> Sisi tuliungana pamoja na kung'oa serikali ya Moi mimi naona uchungu mwingi sana. Walitengeneza katiba ambayo haiwezekani, katiba ambayo ilikuwa ya majimbo... wakati tulitoka Bomas, tulitoka huko na zero yaani 'draft'. Wanataka tupitishe katiba. Kuna yule anaitwa Raila pia kila soko inamwenda wazimu

> wake. Hawa watu walisomea Russia, wamesomea propaganda na vita. Kamotho na Raila wamesomea Russia. Wanasema rais atengeneze katiba. Katiba si kama ugali au chapati. Sio eti Lucy atatengeneza ugali na chapati ili apatie Kibaki awape Wananchi kama hawataki tutaendelea na hii. Martin Shikuku anapiga kelele naye hawezi kuwa hata chairman wa kuchimba mtaro.

Vuta ni kuvute ya katiba ikachacha. Wanasiasa wa pande zote wakatoa maoni yao kuhusu hali hiyo. Kwenye mkutano uliofanyika katika hoteli ya Mt. Kenya Safari Club Bw. Musikari Kombo alikuwa na maoni haya;

> Mambo ya kujitakia makuu yataisha sababu Wakenya wanataka katiba haraka.

Mbunge wa Mandera Mashariki, Mheshimiwa Billow Kerrow, alisema haya kuhusu katiba katika hoteli ya Saphire mjini Mombasa;

> Vitisho vya Mheshimiwa Kiraitu kuhusu LDP ni kuonyesha dhahiri uoga. Nyote munakumbuka kwamba wanachama wa LDP wanaokashifiwa hivi sasa ndio wale wale waliokuwa wakibembelezwa na wanasiasa wa NAK kama vile Kiraitu.

Naye pia mwanasiasa mkongwe wa Mombasa Sharrif Nassir alijiingiza kwa mtafaruku huu wa katiba kwa kunena yafuatayo mkutano wa ziwa la Ng`ombe, Kongowea, Mombasa;

> Nataka kuwahakikishia Wakenya kama hawataki corruption waache katiba ya Bomas ifanye kazi wapende wasipende.

Mzozo wa katiba ilikuwa suala tata na tena telezi ambapo miaka miwili na nusu baada ya uchaguzi katiba mpya nchini Kenya ilikuwa haijapatikana ingawaje wakati wa kampeni Wakenya walikuwa wameahidiwa kuwa katiba mpya itapatikana kabla ya siku mia moja !

## 4.9 Utata wa Lugha Fiche

Wakati huo huo, makabiliano baina ya wanasiasa yalianza, huku wengine wakitafuta mamlaka, ilhali wengine wakikabiliana kwa maneno. Miktadha tofauti ilipelekea matumizi ya lugha kwa njia tofauti wakati shirika la usambazaji wa nguvu za umeme ilipoanza kutekeleza mpango wa kubomoa nyumba zilizokuwa zimejengwa chini ya nyaya za umeme. Bw. Reuben Ndolo aliwachochea watu wa Makadara dhidi ya wafanyi kazi wa kampuni hiyo;

Ndolo: mkiona hao
Wananchi: yaaa
Ndolo: mkiona hao
Wananchi: yaaaaa
Ndolo: weka taya!

Matamshi ya Ndolo hayakuwafurahisha hasa wale wanaoshughulikia usalama wa nchi, na baada ya kuhojiwa na polisi Ndolo alisema;

Mimi si kusema weka taya eti mtu achomwe, nilisema weka taya gari ipite.

Bwana Ndolo hakufungwa jela kufuatia matamshi hayo ya uchochezi. Utata uliopo kati ya maana na fasiri ya lugha ulimnasua mwanasiasa huyu kutokana na uwezekano wa kukabiliwa kisheria, hivyo kudhihirisha dhana ya Obeng (2002) ya

wanasiasa kujinusuru kwa kupitia lugha yenye utata. Lugha fiche iliendelea kutumiwa, huku maana ya lugha hiyo ikiwa inajulikana na vikundi fulani vilivyohusika. Kwa mfano, Ndolo alijitokeza na lugha ambayo watu wa eneo lake la bunge walielewa muktadha na maana barabara.

### 4.10 Nyimbo na Miito ya Siasa

Matumizi ya nyimbo ni mojawapo ya jinsi ya kuwasilisha ujumbe katika jamii. Ingawaje nyimbo wakati mwingine huambatanishwa na ala za muziki na kuchezwa wakati zinapowasilishwa, kuna mifano tofauti ya nyimbo. Nyimbo zingine huwasilishwa kwa ajili ya starehe. Kuna nyimbo ambazo huambatanishwa na shughuli tofauti kwa mfano kuwinda, kulima,vita na kadhalika. Pia kuna nyimbo za tamasha ambazo huwasilishwa kwa ajili ya sherehe fulani ndizo zitakazoshughulikiwa.

Ni dhahiri kuwa nyimbo za kawaida huwasilishwa kwa njia tofauti ili kutosheleza matakwa ya wanasiasa. Nyimbo hizi zinaweza kuimbwa au kutolewa kama miito.Miito na mbinu zingine hutumiwa katika siasa ili kuwasilisha matukio ya kisiasa na sera za wanasiasa na hivyo kuwasilishwa kama matini ya kisiasa. Nchini Kenya nyimbo na miito zilitumiwa na wanasiasa ili kuwasilisha ujumbe waliokuwa nao. Nyiimbo na miito zilitumiwa na pande ya serikali (chama cha KANU) na upinzani ili kuwashinikiza wapiga kura kuweza kupigia chama chao. Wanasiasa hujihusisha na uwasilishaji wa nyimbo na wito ili kuathiri aidha mkondo wa siasa

au hadhira iliyowasikiliza. Hivyo miito na nyimbo ilitumiwa na wanasiasa ili kushawishi wasikilizaji. Miito tofauti iliundwa ili kuhamasisha wananchi kuhusu janga la ukimwi na jinsi ya kujilinda iwapo mtu atafanya mapenzi iyabidi kutumia mipira; kwa mfano mwito kama,

> Ukiona wao, wape kondom
> Weka speed governor
> Wacha kucheza gita ya mwingine.

Hapo masuala kuhusu afya yanazungumziwa ambapo wananchi wanaelimishwa kuhusu ugonjwa usiokuwa na tiba kwa hivyo wananchi wajichunge wasifanye mapenzi ovyo ovyo. Na ikiwa inabidi watumie mipira.

Wanasiasa wengine walijitokeza na mtindo mbalimbali ili kupitisha ujumbe wao. Raila Odinga akajitokeza na matangazo ya mpira na pia kutoa simulizi ambazo hasa wahusika wake wakuu ni wanyama.

> Kuna wale wanapiga kelele kama debe
> Shida haiachi kutaka wanapiga kelele kama tumbili
> anayekaa juu ya miti akifanya ng'ef ng'ef.

Kwa hivyo Raila anatahadharisha wanasiasa wanaomshutumu kuwa wanafanya kazi ya bure.

Kulikuwa pia na matumizi za lugha iliyopambwa kwa nyimbo, au nyimbo zenyewe kupitisha ujumbe fulani. Daktari Mukhisa Kituyi alitumia nyimbo mara nyingi kuwasisimua wananchi katika mikutano ya kisiasa. Lakini nyimbo hizo

hazikulengwa tu kuwasisimua wananchi, bali pia kusuta na kuwakejeli wapinzani. Huu hapa wimbo wake mmoja;

Nilimuliza Uhuru Kenyatta
Rafiki zake akina nani
Alipowataja rafiki zake, ilikuwa ni aibu sana
Mbele yake Arap Moi
Nyuma yake, Ka Biwott
Kando yake vijana wa Mungiki
{Watu wanashangilia}

Nyimbo zilitumiwa kupitishia ujumbe na pia kusuta wapinzani kwa kiasi kikubwa, na zilitumiwa sana na wanasiasa wa chama cha NARC. Wimbo ambao ulitia fora zaidi ni;

Yote yawezekana bila Moi x2
Watoto watasoma bila Moi x2

Ambao ulitoholewa kutoka kwa wimbo wa kidini. Ndolo alipoimba wimbo ufuatao mjini Kitui alijipata mashakani kwani alishikwa na kupelekwa kuhojiwa na makachero. Wimbo uliimbwa hivi;

Watu wa Makadara
Wamechoka na wao
Kina Mwiraria na Chris Murungaru
Bwana Kombo endelea na kazi
Oooooooi ooooooi oooooi
Rais Kibaki ameshindwa na kazi
Mama Lucy endelea na kazi.

Wimbo huu uliwatia Wabunge Ndolo na Owidi mashakani na walitakiwa kuandika taarifa kwa polisi kwa vile ilifasiriwa eti wimbo huo ulimaanisha eti mama Lucy

ndiye Rais wa Kenya. Hii inaonyesha uwezo wa lugha kama chombo cha kuwasiliana na tofauti zilizopo katika kufasiri matini kimuktadha.

### 4.11 Hitimisho

Inadhihirika wazi kwamba wanasiasa hutumia mbinu tofauti tofauti ili kuwasilisha ujumbe fulani. Lugha wanayoitumia inaweza kuwa ya kusuta, kukejeli na hata ya kukashifu. Wanasiasa wanaweza kueleza sera zao kwa kutumia lugha.

# *SURA YA TANO*

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Utangulizi

Sura hii iliaangazia kwa muhtasari matokeo ya utafiti huu pamoja na mapendekezo ya utafiti zaidi na matatizo yalioyokumba utafiti huu.

### 5.2 Matokeo Ya Utafiti

Lengo kuu ni kuwa wanasiasa huwa na lugha yao isiyo ya wazi na hivyo kudhihirisha uneni wao kwa kutumia lugha pinde huweza kuwafanya wao kupata wafuasi wengi. Wafuasi huelewa muktadha unaozungumziwa. Hadhira huelewa historia ya matukio ya awali na hivyo kuweza kung`amua kwa haraka dhana ambayo mwanasiasa anawasilisha kwa wakati mwingi hadhira hufuata msimamo wa wanasiasa.

Utafiti huu umeweza kudhihirisha mambo yafuatayo:

Wanasiasa huimarika kutokana na lugha isiyo wazi anayotumia kueleza maudhui, dhana, kuchochea, kusuta na kupinga. Yote haya yanadhihirisha uwezo wa lugha katika siasa. Kwa hivyo ni dhahiri shahiri kuwa taaluma ya siasa pia ina njia yake ya kuwasiliana.

Matini ya kisiasa huathiriwa na muktadha ambapo kuna hali ya siasa, muundo na matukio. Kulingana na Dijk (1998), njia ambazo wanasiasa hufasiri matukio

yanayoasilishwa. Muktadha hutegemea sababu, malengo na kazi ya matini yote hiyo ili itimike msikilizaji au hadhira lengwa huwa muhimu. Ni kutokana na malengo ya ujumbe katika matini ndipo utakapoelewa ikiwa ujumbe huo ni wa kisiasa au la.

Wanasiasa hutumia ujuzi wa usemi ili kushawishi umma kukubali sera zinazowasilishwa na serikali. Uneni wa kiwango cha juu huwezesha wanasiasa kuonekana kama wabunifu kwa vile ujuzi huu huwasilishwa kwa kutumia tamathali ambazo hufanya wao kuimarika.

Imedhihirika wazi kuwa lugha ya mnato hutumiwa ili kuimarisha umoja baina ya makundi tofauti. Kwa hivyo umoja ukijitenga, lugha hiyo hiyo inaweza kutumiwa ili kuchochea umma ili wachukie sera, dhana na mawazo.

Matumizi bora ya lugha na wanasiasa huwawezesha "kujiuza," kuelezea itikadi zao na sera zao kwa wananchi ili kuomba kura. Richard (1936:45) anaeleza.

> Mwanasiasa aliyeelimika anahitajika kutumia mbinu muafaka ya kuwasilisha hoja, kutumia tamathali murua katika maongezi na yakubalike na umma.

Utafiti umeonyesha kuwa wanasiasa wana mbinu tofauti ya kuhimili mazungumzo ya kisiasa ambapo wanaweza kuongea mambo yasiyo wazi au kukashifu lakini ikiwa ni ya kuhatarisha au ambayo yanaweza kumtia matatani bila shaka huweza kukana kuwa hakumaanisha hivyo. Basi maneno au sentensi za wanasiasa huwa ya undumakuwili.

Uwezo wa lugha hudhihirika pale mwanasiasa hujipatia mamlaka. Uwezo huo uliweza kutumiwa kikamilifu na wanasiasa kujipatia mamlaka kuanzia maeneo yao ya bunge na katika nchi nzima kwa jumla. Kuendelea kutumia lugha kujishikilia kwenye mamlaka waliyopata ni kupitia kwa matumizi ya lugha ambapo mamlaka hayo yalipatikana hivyo kudhihirisha wazi umuhimu wa lugha katika siasa.

Matumizi ya lugha yameathiri maisha ya kila siku ya Mkenya kwa sababu siasa ni maisha na huathiriwa na matukio ya kila siku yanayohusu siasa. Hivyo basi lugha ina uwezo mkubwa wa kuboresha au kuharibu maisha ya watu. Lugha ina uwezo wa kuunganisha watu au kuwatawanya, kuleta amani au vita, kujenga au kubomoa jamii.

Lugha iliyotumiwa na chama cha NARC ilisheheni matumaini na kuashiria maisha mapya kwa Wakenya, ambao walijitolea mhanga na kukipigia chama hicho kura. Ahadi zilizotolewa na chama hicho ndizo chanzo cha matumaini yaliyopelekea wananchi kukipa mamlaka.

Uwezo wa lugha katika matini ya kisiasa nchini Kenya ulipelekea kuchochea wananchi dhidi ya chama cha KANU ambacho kiliaminika kuwa kilitumia kiasi kikubwa cha pesa kujaribu kupata wafuasi. Hatima yake ni kuwa lugha ilikuwa na uwezo mkubwa.

Lugha ilitumiwa kuathiri mafikira ya watu, mabadiliko ambayo yalileta pia mabadiliko katika jamii kwa jumla. Serikali mpya ya NARC ilikuwa zao la uwezo huo. Uwezo huo wa lugha ulizaa sera mpya za kusimamia maisha ya Wakenya. Chama cha KANU hakikuwa na nafasi kwani lugha iliyotumiwa na wapinzani wake ilididimiza matumaini yoyote ambayo chama hicho kingekuwa nayo. Kilichorwa kama chama cha wezi, wauaji, waporaji na wanyanyasaji. Matumaini yakawa katika chama kilichoahidi ufanisi katika nyanja zote za maisha. Yote haya yaliwezekana kwa sababu ya uwezo wa lugha.

Uwezo wa lugha haujajikita tu katika maneno yanayotumiwa, bali pia mahali maneno hayo yanayotumika na hadhira iliyopo. Wanasiasa hutumia lugha kufaa miktadha mbalimbali ili kuweza kutimiza lengo lao kuu, ambalo ni kupata mamlaka sio tu kwa kutoa ahadi zinazovutia zaidi bali pia kwa kubomoa wapinzani.

Baada ya uchaguzi mkuu, serikali mpya ilitumia lugha ili kuelezea mikakati mipya itakayotumia. Ilitumia lugha pia kuelezea sera zake na kuwalazimisha watu kufuata sera hizo, kwa sababu lugha huelezea mahusiano yale yaliopo baina ya serikali, watu na sera hizo. Lugha imekuwa chombo cha kupigania vita vya kujikomboa, ambapo adui ni umaskini, ujinga, magonjwa na unyanyasaji. Silaha ni utawala mzuri, bidii ya wafanyikazi, sera nzuri na amani. Makamanda ni viongozi nao askari ni wananchi. Ushindi ni mafanikio katika nyanja zote za maisha.

Kilichodhahiri ni kuwa lugha iliyotumiwa na wanasiasa imedhihirisha tofauti mbalimbali zilizopo baina ya mbinu za matumizi ya lugha baina ya wanasiasa. Kwa kiwango kikubwa, tunaweza kugawanya lugha iliyotumika katika kipindi hicho (2002-2005) katika matapo mawili- lugha ya kabla ya uchaguzi, na lugha baada ya uchaguzi mkuu wa 2002.

Lugha kabla ya uchaguzi mkuu ilisheheni ushawishi mwingi huku wanasiasa wakisihi wananchi wawapigie kura. Kushawishi huko kulilengwa kupata usikivu wa wananchi ili maswala yaliokuwa yameibuka yapate wasikilizaji. Swala kubwa lilikuwa ubadilishaji wa serikali, hasa katika uongozi wa nchi. Kwa sababu lugha tamkwa ina uwezo mkubwa wa ushawishi, huwa inaathiri tabia na mafikira ya watu kwa kiasi kikubwa.

Wanasiasa kadhaa walijitokeza kuwa maarufu hasa kwa sababu ya nguvu iliyojikita katika lugha yao. Hawa walionyesha umaahiri mkubwa katika kumudu lugha kwa mapana na marefu. Bw. Michael Kijana Wamalwa, kama vile tulivyoona hapo awali, alijua kutumia lugha iliyolazimisha watu kuisikiliza. Lugha iliyopambwa kwa mtiririko wa mawazo na msamiati teule uliofunikwa kwa lafudhi ya wenyeji wa lugha hiyo, ndipo hasa alipoitwa mtu anayezungumza Kiingereza cha Malkia wa Uingereza.

Kipindi hicho pia kilishuhudia matumizi ya lugha iiiyofichwa na iliyovishwa 'buibui' ili kupunguza makali ya matamshi halisi. Lugha fiche huwapa watu jambo la kufikiria na pia huzuia aibu kubwa inayoweza kuwapa wale ambao wanatajwa hasa kama wako katika hadhira.

Matumizi ya misemo mbalimbali yalikuwa si nadra katika lugha ya wanasiasa wengi. Misemo ilitumiwa sio tu kwa kurembesha lugha bali pia kwa kutoa mafunzo maalum kulingana na matukio mbalimbali. Kulikuwa na matumizi ya sitiara na urejeleaji wa historia. Matumizi ya lugha ya heshima pia yalikuwepo hasa pale wananchi au viongozi mashuhuri walipolengwa. Maneno hayo ni kama vile mheshimiwa na Wananchi watukufu. Kuna wanasiasa wengine waliotumia lugha kishairi ili kuchangamsha wafuasi na kurembesha mazungumzo yao ili yawe ya kuvutia zaidi.

Wanasiasa wengi walionyesha kujali hisia za kadhira na kuwa hivyo lugha yao ikawa imelenga kujali maslahi ya hadhira kama vile uchovu, jua au baridi kali. Hivyo lugha ikatumiwa ambayo iliwafanya wafuasi kusubiri hadi tamati za mikutano. Maneno kama sitachukua mda mrefu au mwisho kabisa yalitumiwa na wanasiasa wengi. Kulikuwa pia na matumizi ya viwakilishi badala ya kutaja majina kamili ya mtu au kitu. Matumizi hayo lugha huwa yananuiwa kupunguza migogoro au migongano baina ya watu au wanasiasa.

## 5.3 Mapendekezo

Utafiti zaidi unahitajika kufanywa kuhusu mwingiliano uliopo wa matini za siasa nchini Kenya. Nafasi ya nyimbo na miito nchini Kenya ili kuleta mageuzi pia yafaa ifanyiwe utafiti zaidi kwa vile haijabobewa. Litakuwa jambo murua ikiwa utafiti zaidi utafanywa kuhusu hotuba za Marais wa Kenya kwa mfano Hayati Kenyatta, Rais Mstaafu Moi na hata Mheshimiwa Kibaki.

## 5.3 Matatizo

Utafiti huu ulikumbwa na matatizo kadha wa kadha. Baada ya kuteua sampuli tulipoenda nyanjani hotuba za wanasiasa wengine zilikosekana kwenye studio. Ilibidi kuteua wanasiasa wengine ili kuchukua mahali pa sampuli za awali zilizokusudiwa.Tuliopata matini ya mwanasiasa mmoja kutoka Kaskazini Mashariki.

Kwa vile mashirika haya hutekeleza wajibu mkubwa wa kupasha umma habari yana wafanyikazi wengi ambapo studio hujaa kila mara hivyo kuzua tatizo la kutumia mashine ambapo watu ni wengi ilhali mashine ni chache. Ilinibidi kubadilisha ratiba na hivyo kwenda studio siku za jumamosi na jumapili tu.

Gharama za utafiti katika mashirika haya ya utangazaji ni ghali kwa kuwa mtafiti analipa ada ya maktaba na studio.

## RATIBA

| TAREHE | MATUKIO |
|---|---|
| 1 hadi 29<br>Novemba 2004 | Kuandika pendekezo |
| 30 Novemba 2004 | Kuwasilisha pendekezo kwa msimamizi |
| 8 hadi 30<br>Desemba 2004 | Kuwasilisha pendekezo kwa mkuu wa idara |
| 6 Januari 2005 | Uwasilishaji wa pendekezo kwa idara |
| 15 Januari 2005<br>(kuendelea) | Kurekebisha pendekezo |
| **Jumatatu**<br>$7^{th}$ Februari 2005<br>14, Februari 2005<br>21 Februari 5005<br>$28^{th}$ Februari 2005 | Kutembelea maktaba ya Shirika la Utangazaji la Nation na kusoma magazeti ya Nation na Taifa Leo. |
| **Jumanne**<br>1 Februari 2005<br>8 Februari 2005<br>15 Februari 2005<br>22 Februari 2005 | Kusoma magazeti ya Standard |
| **Jumatano**<br>2 Februari 2005<br>9 Februari 2005<br>16 Februri 2005<br>23 Februari 2005 | Kusoma magazeti ya Standard |
| **Alhamisi**<br>3 Februari 2005<br>10Februari 2005<br>17Februari 2005<br>24 Februari 2005 | Kusoma katika maktaba ya chuo kikuu cha Nairobi |

| | |
|---|---|
| **Ijumaa**<br>4 Februari 2005<br>11Februari 2005<br>18 Februari 2005<br>25Februari 2005 | Kusoma maktabani katika Chuo kikuu cha Kenyatta |
| **Jumamosi**<br>5 Februari 2005<br>12 Februari 2005<br>19 Februari 2005<br>26 Februari 2005 | Ukusanyaji wa data kwa kuangalia kanda za video. |
| **Jumapili**<br>6 Februari 2005<br>13 Februari 2005<br>20 Februari 2005<br>27 Februari 2005 | Ukusanyaji wa data kwa kuangalia kanda za video. |
| 15/3/2005 mpaka 23/4/2005 | Kuchanganua na kuandika tasnifu |
| 03/05/2005 | Kuwasilisha idarani |

## Marejeleo


Austin, J. (1975) *How to Do Things with Words*, Chicago; Oxford University Press.

Bakhtin M. (1981) *The Dialogic Imagination; Four Essays*, Austin: University of Texas Press.

Beugrade R. na W. Dressler (1981) *Introduction to Text Linguistics*; New York; Longman.

Boomaert J. (1990) *Modern Africa Political Style: Strategies and Genre in Swahili Political Discourse. In Discourse and Society;* London: UK

Bright W (1992) *International Encyclopedia of Linguistics;* Oxford: Oxford University Press.

Brown G. na G. Yule (1983) *Discourse Analysis*, Cambridge; Cambridge University Press.

Busman H. (1996) *Routhedge Dictionary of Language and Linguistics;* London: Thomsom Publishers Company.

Chilton P. na C. Schaffner (1997) *Discourse and Politics;* London; Sage Publication.

Chilton P. na M. Ilyin (1993) *Metaphors in Political Discourse*; London; Sage publication.

Crystal D. (1987) *The Cambridge Encyclopaedia of Language,* Cambridge: Cambridge University Press.

Crystal D. (1969) *Investigating English Style,* London; Longman.

Coulthand M. (1977) *Introduction to Discourse Analysis,* London; Longman.

Dijk T (1977) *Text and Context; Explorations in the Semantics & Pragmatics of Discourse,* London; Longman.

Dijk T.(1998) *Principles in Critical Discourse Analysis in the Sociolinguistics. Reader Vol.2 Gender and Discourse,* New York; Oxford University Press.

Edelman M (1977 ) *Political Language; Words that Succeed and Policies Facts,* London; London Press

Fairclough, N (1989) *Language and Power,* New York; Longman Group Ltd.

Foucalt M. (1997) *The Archeology of Knowledge,* New York; Basic Books.

Halliday M. na R. Hassan (1976) *Cohesion in English,* London; Longman

Habwe J. na P. Karanja (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili,* Nairobi; Phoenix Publishers.

Habwe H.J. (1989) *Pragmatiki Katika Mazungumzo ya Kawaida, Kimvita,* Unpublished M.A. Thesis, University of Nairobi.

Habwe H.J. (1999) *Discourse Analysis of Swahili Political Speeches,* PHD Thesis, University of Nairobi.

Haugerud A na S.K. Njogu (1991) *State Voices in the countryside: Politics and the Kenyan Baraza,* African Studies Center,Boston; Boston University.

Lakoff G. (1990) *Talking Power; The Politics of Language, Chicago;* Basic books.

Lakoff G. (1992) *Metaphors and War,* Philadelphia; Benjamins Publications.

Lakoff G. na M. Johnson (1980) *Metaphors We live by,* Chicago; Chicago Univeristy Press.

Lasswell, H. D. (1936) *Politics; Who Gets What, When, How,* New York; Mcraw Hill

Leech Geoffrey (1970) *Towards a Semantic Description of English,* London; Longman

Leech Geoffrey (1969) *Principles of Pragramatics,* London; Longman

Lwaitama A.F. (1988) *Variations in the Use of Personal Pronouns in the Political Oratory of J.K. Nyerere and A.H. Mwinyi,* Dar es Salaam; University of Dar es Salaam

Lwaitama A.F. (1995) *A Critical Language Study of Tanzania Kiswahili Presidential Political Oratory PhD Thesis,* Birmingham Department of modern languages, Aston University in Birmingham, U.K.

Mesthrie R. (2000) *Introducing Socio-linguistics,* Edinburgh; Edinburgh Press.

Michira J.N. (1993) *Uchanganuzi wa Kimtindo wa Lugha ya Wachuuzi na Lugha ya Matangazo ya Biashara Redioni.* M.A. Thesis; University of Nairobi.

Morgan G. (1980) *Paradigm, Metaphors and Puzzle Solving in Organization Theory,* London; London Press.

Msanjila Y.P. (1989) *Socialinguistic Rules of Formal Address in Kiswahili. In D.P.B. Massamba et al* (ed) Jarida la Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili vol. 56; Dar-es-Salaam; TUKI.

Mohammed S.A. (2001) *Mwongozo wa Kilio Cha Haki,* Nairobi; Longhorn Kenya Ltd.

Msokile M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi,* Nairobi; East African Educational Publishers

Murray E. (1977) *Political Language;* Florida; Academic Press Inc.

Mugenda O. na E. Mugenda (1999) *Research Methods; Quantitative and Qualitative Approaches,* Nairobi; Acts press;

Neyole E. (2003) *"Umatini katika Vichekesho vya Redykyulass."* "Tasnifu M.A. chuo kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa).

Ngoyani G. (2002) *Ujamaa (Socialism) Metamophors; The Basics of President Nyerere's political terminology, New York;* Nova Science Publishers.

Njue J.G. (1989) *Muwala Katika Kiswahili: Umuhimu wake katika Uchambuzi wa Ngano za Waswahili,* Unpublished M.A. Thesis. University of Nairobi

Ogula P. (2002) *Research Methods,* Nairobi; Catholic University of Eastern and Central Africa.

Obeng S. G. na B. Hartford (2002) *Surviving Through Obliqueness; Language of Politics in Emerging Democracies, New York; N*ova science Publishers, Inc.

Reeves F. (1983) *British Racial Discourse. A Study of British Political Discouse about Race and Race Related Matters;* Cambridge; Cambridge University Press.

Richard J. (1985) *Longman Dictiionary of Applied Linguistics,* Edinburgh University Press.

Richard I.A (1936) *The Philosophy of Rhetoric,* Oxford; Oxford Univerity Press

Salkie R. (1995) *Text and Discourse Analysis,* London; Routledge.

Scotton C.M (1993) *Social Motivation for Code Switching- Evidence from Africa,* Oxford; Clarendon Press.

Steinhart E. na E. Kittany (1998) *Metaphor in J. Mey & R. Asher, Concise Encyclopedia or Programatics; New York;* New York Elservier .

Todd L. (1989) *An Introduction to Linguistics,* London; Longman

Tuki (1990) *Kamusi Sanifu ya Lugha na Isimu,* University Press of Dar-es-Salaam.

Wales K. (1991) A *Dictionary of Stylistics,* London; Longman.

Wamitila K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Dhana,* Nairobi; Focus Books

Wamitila K.W. (2003) *Kichocheo cha fasihi simulizi na andishi,* Nairobi; Focus Books

www.estandard.com *Standard Newspapers*

www.nationmedia.co.ke *Nation Newspapers*

Yankah K. (1995) *Speaking for the Chief;Indiana;* Indiana University Press.

Yahya Othman S. (1994) *Covering one's Social Back. Politeness Among the Swahili In TeunVan Dijk* (ed)text and Interdisciplinary Journal for the study of Discourse. New York; New York de Gruyter.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY